# *KUFANYA MAKONGAMANO*

Asanteni sana.

2 Mnaweza kuketi. Bila shaka tuna furaha kuwa hapa usiku wa leo kwenye usiku huu wa tatu wa ninii, kongamano hili kuu. Nami nilikuwa nikizungumza na Ndugu Weston na Ndugu David du Plessis, tulipokuwa tukitoka, juu ya ma—maendeleo ya Kanisa siku hizi, jinsi ambavyo Mungu anatenda kazi miongoni mwa madhehebu yote, na kuwaleta watu nje wakiona njaa na kiu kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Kwa kweli tunashukuru kwa ajili ya mambo haya.

3 Na sasa, nilikutana na mtu fulani nikiingia pale, akanipa mkono. Akasema, "Ndugu Branham, kamwe sikupata nafasi ya kukutana nawe," akasema, "lakini, ama, kuzungumza nawe, lakini," kasema, "niliponywa katika mkutano wako huko Palm Beach," ninaamini ndiko, mahali fulani. Loo, ni—nitakisia nitakapovuka mto, natumaini kuona maelfu ya wale ambao wamekuwa . . .

4 Wakati mwingine hapa, maisha yanakuwa sana sana, loo, sijui, una—unakuwa na haraka, na una pilikapilika na hekaheka na patashika, kama mama alivyozoea kusema, na karibu unajikuta ukirudi. Wala sioni tuna haraka hivyo kwa nini hata hivyo, mnaona, hatufanyi zaidi ya walivyofanya katika siku za Moody, na Finney, Knox, na Calvin. Walipanda farasi na mkokoteni, nao wakafanya maskini mkutano wa kambi kama huu, na kupiga hema huko mwituni, na kula kuchakulo kama kiamshakinywa, na maharagwe yaliyoganda jioni, na ilikuwa sawa. Unakumbuka hilo, Ndugu Sullivan? Huko nyuma kabisa katika siku hizo za kale, huko chini Kentucky?

[Ndugu Sullivan anasema, "Naam, bado ninawapenda."—Mh.]

5 Nami pia, Ndugu Sullivan; hakika wao ni wazuri. Sote wawili ni Wakentaki na tuna mambo mengi shirika, jamaa huyu hapa pembeni. Naye alifikiri alikuwa amenipata nilipokuwa hapa mara ya mwisho, kasema, "Nina hakika, hujui hirizi ni nini?"

6 Nikasema, "Usiniambie sijui. Ni—nilibeba fusho lake shingoni mwangu shuleni mpaka mimi . . . hata hakuna mtu angeketi karibu nami. Hakika najua."

7 Ni wangapi wanaojua ni nini? Vema, waangalie Wakentaki hapa, sivyo? Ndugu Banks Wood, uliinua mkono wako, popote ulipo? Vema, naona ulikuwa, hilo ni sawa, ni jambo jema uliinua. Ndugu Wood alikuwa mmoja wa watu waliokuwako, yeye na

ndugu yake pale, wakati yule samaki mdogo alipofufuka siku hiyo, ali—alikuwepo.

8 Vema, sote tunaninii . . . Ikiwa nyote mna wakati mzuri hapa nje kwenye uwanja wa kambi kama nilivyo mimi, mbona, huku tukiwatembelea watu na kadhalika, tuna wakati mzuri sana. Na sasa, nafikiri tunapaswa tu kufanya kila chembe ya mkutano huu itumike kwa utukufu wa Mungu, kila chembe yake tu.

9 Sasa, ninasikia kuunga mkono na kupinga, wengine wakisema tunapaswa kuwa na usiku wa kuwaombea wagonjwa, na wengine wakisema, "Ndugu, kamwe usiyakomeshe, jinsi nafsi yangu inavyofurahia mlo, vinginevyo." Kwa hiyo, sijui, lakini nafikiri tunapaswa kuwa na usiku wa maombi kwa ajili ya wagonjwa, na kuwaombea.

10 Mnajua, watu wamefundishwa kwamba inatupasa kuwawekea wagonjwa mikono, kwangu mimi, jinsi ninavyoliona, ni—ninajua tu mradi Roho Mtakatifu yupo, kazi imekamilika, mnaona. Hivyo—hivyo tu, imekwisha.

11 Na hivyo ndivyo tunavyoliona huko ng'ambo, Ndugu Mattsson, kwamba sisi . . . mradi tu wanaweza kuona jambo fulani likitukia, kama wanajua ya kwamba nguvu za kimbinguni za Mungu ziko karibu, watalikubali tu, wasimame moja kwa moja, waondoke. Kama wao . . . Huenda wakayumbayumba kwa muda, kama wanatoka kwenye kiti cha magurudumu, ama kitu fulani, bali wataendelea kusonga mbele mpaka watakapoanza kwenda. Na kwa hiyo wao . . .

12 Lakini hapa, inaonekana kana kwamba karibu inakubidi kuwawekea watu mikono, wamefundishwa hivyo. Sasa, kama utaninii . . . Sasa, hilo ni sawa, hilo ni sawa kabisa, lakini kama mtanivumilia, katika Maandiko hayo yalikuwa ni mapokeo ya Kiyahudi ya kuwekea mikono. Sasa angalieni, wakati binti Yairo alipokuwa mahututi, Yairo alisema, "Njoo umwekee mikono, naye ataishi." Mnaona, mapokeo ya Kiyahudi.

13 Lakini alipoenda kwenye nyumba ya Mmataifa, ambapo mtumishi wake alikuwa amelala mahututi, alisema, "Sistahili kwamba Wewe uje chini ya paa langu, wala sikujihesabu ninastahili kuja Kwako." Hiyo ndiyo sababu alimtuma mtu fulani kumwambia. Kasema, "Nena tu Neno, mtumishi wangu ataishi." Akasema, "Kwa kuwa mimi ni mtu niliye chini ya mamlaka, na nikimwambia mtu *huyu*, 'Nenda,' anaenda; na *huyu*, 'Njoo,' anakuja." Kwa maneno mengine, "Kila kitu kilicho chini ya mamlaka yangu hakina budi kunitii."

14 Naye alikuwa akisema nini, Mmataifa kwa Yesu? "Ninatambua ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, na magonjwa yote yako chini ya mamlaka Yako, unaweza kuuambia, 'Nenda,' nao hauna budi kuondoka." Unaona?

15 Kila kitu kilicho chini ya mamlaka Yake ni—ni . . . Naye alitambua kwamba ugonjwa, na dhambi, na kila kitu

kilikuwa chini ya—chini ya mamlaka Yake, kwamba angeweza kuvidhibiti. Sasa, nafikiri hivyo ndivyo tunavyopaswa kuliona siku hizi, nimejaribu kwa miaka mingi. Lakini mnaona, kile kinachosababisha jambo hilo, kuna ndugu wengine wengi hudumani, nao wanawawekea wagonjwa mikono na wanapata mafanikio makubwa.

16 Na kwa njia hiyo, niliichambua tu, nami nikaacha yapata mwaka mmoja uliopita, na kusema, "Vema, vema, mradi tu niko Marekani, tutawaombea tu wagonjwa, tuwawekee mikono, hiyo ni kweli kabisa," maana naona inaleta matokeo bora zaidi.

17 Lakini kweli kwa kweli: Kama Roho Mtakatifu anaweza kusimama hapa na kupitia kwenye kusanyiko hilo huko nje, na kufanya kazi zile zile alizofanya wakati alipoishi katika mwili unaoitwa Yesu Kristo, anaweza kukupa imani ya kuamini, nami karama ya kuthibitisha, ya kwamba ni Uwepo kabisa wa Roho Mtakatifu, kwangu mimi, kazi imekwisha, tangu Kalvari, imekwisha. Na sasa amini tu na uendelee kulitekeleza, usininii tu—usiwe na chochote cha zaidi kuliwazia, ninii tu, imekwisha na ni hivyo tu. Mungu alisema hivyo, na hilo linalitatua.

18 Ninaendelea kuzungumza, vema, mtaganda usiku wa leo, mkiketi huko nje, sivyo? Hii ni hali nzuri ya hewa hapa juu, afadhali niwe nayo hivi, halafu ingekuwa joto sana, mngekuwa tu mmeketi hapo mkijipepea, kwa nguvu tu mwezavyo kujipepea.

19 Kwa hiyo sasa ninataka kusoma usiku wa leo kutoka kwenye Maandiko kwa ajili ya somo, nami nitajaribu kuwaachilia upesi iwezekanavyo. Lakini kabla sijafanya hivyo, ni wangapi wangefikiri ingekuwa vizuri kuwa na u—usiku wa uponyaji moja kwa moja? Ningependa tu kuona kama ni kutaka kwa watu. Sasa, inueni mikono yenu, ninyi mnaofikiria tunapaswa kuwa nayo moja kwa moja. Vema. Inaonekana kana kwamba tunapaswa kuifanya moja kwa moja, sivyo? Hakika, yapata asilimia tisini na tano.

20 Vema, tutakuwa na ibada ya uponyaji kesho usiku basi. Vipi hivyo? Hiyo ni sawa? Tutakuwa na ibada ya uponyaji kesho usiku, ama, kuwaombea wagonjwa, hatujui Mungu atafanya nini, hatutasema watu wataponywa. Mimi . . . Daima wamekuwa hivyo, bali tutamtumainia tu Mungu kwa ajili ya wagonjwa kesho usiku. Vipi hivyo? Nami nita—nitawaombea kesho usiku.

21 Na sasa kesho alasiri, ninaamini, kwa kuwa kuna wengi sana, ninaangalia . . . Mimi sina uwezo sana wa kukadiria, ningesema kuna angalau watu elfu mbili, au zaidi, hapa. Na kwa hiyo katika hilo, kungekuwa na kama elfu moja mia tano hapa, ama zaidi, wa kuombewa endapo kuna watu elfu mbili. Halafu basi kungekuwa . . . Kulikuwa na . . . Hao watakuwa ni wengi sana, na ingekuwa ni kusukumana na kufinyana, kwa hiyo huenda ikatubidi kuchukua kesho usiku, na usiku unaofuata.

22 Niliwazia katika kongamano, ningezungumza tu na watu kama wangeweza kuvumilia hilo. Halafu baada ya kongamano kwisha, nina siku mbili usiku za kukaa tu hapa na kuwaombea wagonjwa, na hiyo ni Jumamosi na Jumapili. Na hivyo ndivyo nilivyokuwa ninaenda kufanya, na kutumia tu hii kuwaita madhabahuni.

23 Sasa, mimi . . . ninataka kusema jambo hili, kwamba nafikiri ya kwamba uponyaji wa Kiungu ni jambo kuu, ni moja ya sifa za Mungu, ninaamini hilo, kuwaponya wagonjwa. Lakini ninaamini ya kwamba wokovu wa nafsi ni zaidi ya uponyaji wowote wa Kiungu, mnaona, umeupita kwa mbali sana. Nami niliona hivi majuzi usiku, nilipouliza ni wenye dhambi wangapi waliokuwapo, kulikuwa tu na wanne ama watano, nao walikuja hapa na kusimama kwa ajili ya wokovu.

24 Halafu basi, kama wewe ni . . . kama bado hujampokea Roho Mtakatifu, sikiliza, ndugu yangu mpendwa, kadiri watu wanavyoupinga mara nyingi kwamba si wa siku hizi, ni wa siku hizi, mnaona, Roho Mtakatifu. Nawe usiondoke kwenye uwanja huu wa kongamano mpaka umempokea, wewe dumu moja kwa moja na Mungu. Endelea tu . . .

25 Usi—usi—usitengeneze njia yako, jinsi unavyotaka kumpokea, unaona, unalo niani mwako ya kwamba huna budi kuona kitu fulani, ama kuwa na mhemuko fulani. Unapoingia mle ndani kuomba, wewe ingia tu ukisema, "Bwana, nimekuja kumpokea Roho Mtakatifu." Unaona? Naye atashughulikia yaliyosalia. Kuwa tu—kuwa tu mwaminifu kabisa, vunja mawazo yote ya kwamba hutampokea. Kumbuka, usiku wa leo ndio usiku utakaoupokea. Unaona? Ni hayo tu.

26 Kama ilivyokuwa kwa mzee fulani, siku zilizopita, a—asingeweza—asingeweza kudumisha wokovu, a—angeokoka, halafu baada ya kitambo kidogo angefanya kosa, ibilisi aseme, "Unaona, kamwe hukuokoka."

27 Vema, hilo liliendelea kwa muda mrefu. Basi siku moja, akatoka akaenda kondeni, akaomba kwa bidii tena, akasema, "Mimi, Bwana, na—na—najua Wewe uliniokoa." Kwa hiyo, akasema, "Shetani, nitakufanyia jambo fulani."

28 Ndipo akaondoka akaenda akajitwalia shoka, akajikatia kijiti kikubwa mno, kirefu, akakishindilia chini ardhini, na kusema, "Shetani, kama wakati wowote ukinijia na kuniambia sijaokoka, nitakurudisha moja kwa moja nyuma na kukuelekeza kwenye kijiti hiki, papa *hapa* ndipo lilipotukia." Unaona? "Nimeokoka tangu sasa na kuendelea."

29 Sasa, pigilia tu chini kijiti usiku wa leo, useme, "Shetani, kutoka papa *hapa* ndipo nitakapokaa kwenye kizingiti hiki mpaka—mpaka Mungu atakaponipa Roho Mtakatifu. Hutamwondoa kwangu, tena, na, au, kuondoa mawazo yangu

kwangu, kunifanya nifikiri nimechoka sana, ama ninapaswa kufanya jambo lingine."

30 Mradi una mawazo hayo, kamwe hutampokea. Huna budi kuingia mle ukisema, "*Huu* ndio wakati nitakaompokea, *huu* ndio wakati wangu." Ndipo basi utampata.

31 Wewe, makinika kabisa na Mungu, naye Mungu atakuwa makini nawe kabisa. Hiyo ni kweli. "Nikaribieni, nami nitawakaribia, asema Bwana."

32 Vema, kesho usiku, Bwana akipenda, nitamtuma Billy Paul, mwanangu, hapa nje ku—kugawa kadi za maombi kwa ajili yenu ninyi watu mnaotaka kuombewa. Na ni wangapi waliopo hapa kutoka nje ya jimbo sasa, ambao wataombewa, ama nje ya mji walioko hapa uwanjani? Hebu tuone mikono yenu. Loo, kuna wa kutosha kwa ajili ya kadi nyingi za maombi. Kwa hiyo, atazigawa mapema ili isiingilie sehemu iliyobaki ya mkutano. Ni wakati gani ninyi kwa kawaida. . .wanapoanza kukusanyika, Ndugu Sullivan?

[Ndugu Sullivan anasema, "Vema, kuanzia saa kumi na moja na kuendelea, Ndugu Branham."—Mh.]

33 Vema, kuanzia saa kumi na moja hadi saa kumi na mbili na nusu basi, njoni hapa na—nasi tutagawa kadi za maombi kesho usiku, na kuitisha mstari, na kuwaombea wanapopita jukwaani.

34 Sasa, fungu hili, usiku wa leo, ni fungu la kipekee sana, na hata hivyo, ni fungu zuri sana kwa. . .na fungu linalojulikana sana. Lakini linapatikana katika Isaya, mlango wa kwanza na kifungu cha 18. Nami ninaamini, hebu na tusome vifungu vichache kabla ya hapo, na kufanya tu. . .tuone kama tunaweza kupata muktadha kutoka kwake. Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 15, ama cha 16, labda iwe mbele zaidi:

> *Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele ya macho yangu; acheni kutenda mabaya;*
>
> *Jifunzeni kutenda mema; itafuteni hukumu, wasaidieni walioonewa, mpatieni yatima haki yake, mteteeni mjane.*
>
> *Haya, njoni,. . .tusemezane, asema* B*WANA*, *dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana,* hata hivyo *zitakuwa. . .nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.*

35 Na sasa, kama ningeliita hili somo, kutoa muktadha kutoka kwake, ningeliita kile ninachotaka kuzungumzia usiku wa leo ni *Kufanya Makongamano*. Basi hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya kongamano pamoja na Mungu kabla hatujaendelea mbele zaidi.

36 Baba yetu mwenye rehema na upendo sana, Mungu wa uhai wote, uliyemtuma kwetu Mwanao mpendwa, Bwana Yesu, ili Yeye apate kuwa kipatanisho cha ninii zetu. . .cha dhambi zetu,

akatwaa juu Yake mfano wa mwili ulio wa dhambi, akafanywa dhambi kwa ajili yetu ili sisi watu wasiostahili tuweze kuvutwa karibu na Mungu, kwa kumwagwa kwa Damu Yake mara moja tu.

37 Nasi tumekusanyika hapa katika kongamano hili, Bwana, katika siku hizi usiku, sio tu kuonekana na wengine, ama hata kushirikiana sisi kwa sisi. Bwana, tunaomba ya kwamba kama huo umekuwa ndio mtazamo wa watu hadi wakati huu, na mimi mwenyewe, kwamba Wewe utatusamehe dhambi yetu.

38 Tumekuja, Bwana, katika wakati wa kufa, tumekuja katika wakati ambapo tunajisikia hatuna muda mwingi uliosalia, nasi tumekusanyika hapa kwa kusudi moja, na hilo ni kuwa karibu na Wewe. Tunataka dhambi zetu chini ya Damu, tunataka ushirika wa karibu, tunataka kulizungumzia na Wewe, Bwana, kabla hujaja, kwa kuwa siku hiyo, itakuwa imechelewa sana basi.

39 Nasi tunaomba usiku wa leo, Baba Mungu, ya kwamba utaweka njaa kubwa sana katika mioyo ya watu mpaka kote juu na chini ya kingo hizi za mito kutakuwa na mikutano ya maombi ikiendelea, watu wakimtafuta Mungu katika hali ya kudhikika, wakijua ya kwamba hawana budi kupata raha nafsini mwao na kumpokea Roho Mtakatifu, la sivyo siku moja watatumbukia katika Umilele bila kukujua Wewe. Ee Mungu, uturehemu.

40 Na tunapoona makanisa yetu katika makundi yetu wenyewe ya Full Gospel yakianza kupoa, na inaonekana kana kwamba hakuna kilio kikubwa kwa ajili ya nafsi zilizopotea, hakuna tena maombi hayo maaminifu ya usiku kucha na kulitafakari Neno. Na inaonekana kama ndio kwanza tuteleze tu, Bwana. Tusamehe, Ee Mungu, na jalia tujifanye upya usiku wa leo, upya katika Roho Mtakatifu.

41 Nasi tunaweza kuwazia juu ya siku zilizopita, katika wakati wa Wamethodisti, walipoomba usiku kucha na kulia kwa machozi ya uchungu kwa ajili ya waliopotea, wala hawakuwa na amani, na usiku wa leo inaonekana kana kwamba tunaweza kuvaa vizuri, na kuketi chini na kusikiliza, na kwenda nyumbani bila kujali. Ee Bwana, chochea mioyo yetu usiku wa leo, weka bidii ndani yetu kwa ajili ya nafsi zilizopotea. Jalia wahudumu na walei, kila mtu kufanyika sehemu ya Ufalme na tukiwa na shauku kubwa, mpaka tutakapoitembelea miji, na kila mahali, na kuvuta waliopotea kutoka kwenye mifereji ya maji, na—na kuwachukua kama kinga za moto kwa ajili ya Bwana. Tujalie, Baba.

42 Tunasoma katika Kitabu ya kwamba inasemekana ya kwamba Malaika alitoka akaenda na kuweka alama juu ya wale waliougua na kulia kwa ajili ya machukizo yaliyofanywa katika mji huo. Tukitambua kwa Maandiko, huko kulikuwa ni kuja kwa kwanza kwa Roho Mtakatifu kupitia mji wa Yerusalemu, na halafu kurudi Kwake mara ya pili, katika, wakati huu wa

kuwaita watu kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake, ni zaidi sana jinsi gani tunapaswa kuhusika, na kuugua, na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa!

43 Tunaona makanisa yakicheza roki, na kucheza karata, na kuwa na mashindano ya kuogelea ya kila namna, na kadhalika, kanisani, huku mikutano ya maombi na mikutano ya kukesha usiku kucha imesahauliwa. Mungu, turudishe kwenye kitu kilicho halisi.

44 Jalia Roho Mtakatifu aje miongoni mwa watu hawa usiku wa leo, Bwana, na kuanzisha Pentekoste papa hapa. Tujalie, Bwana, katika kila moyo, kweli wanataka kufanya hivyo, liko mioyoni mwao kufanya hivyo, lakini shughuli za ulimwengu na wepesi wa kupita kwa wakati umewarai wakatoka. Bwana, anza kutoka kwenye mimbara hii, kutoka kwangu, na uende kwenye kusanyiko, na kusonga mbele kuliko hapo awali, na kutupa bidii kwa ajili ya nafsi zilizopotea. Tujalie, Bwana.

45 Maoni haya yatakayotolewa kwenye Neno, kama ni mapenzi Yako, tunaomba ya kwamba yatakuwa mbegu mioyoni mwa watu kujibu maombi haya kwa ajili ya mtumishi Wako. Tujalie, Bwana. Tunaamini, nami ninaamini kwa moyo wangu wote kama mkutano kama huo ungetokea kwenye uwanja huu, kwamba ingekuwa ni ibada ya daima ya uponyaji wakati wote. Shetani na nguvu zake asingeweza kukaa katika kundi takatifu kama hilo. Tujalie, Bwana.

46 Ninayakabidhi yote Kwako, na kukungojea Wewe unene Maneno sasa, na kumwacha Roho Wako Mtakatifu alifasiri kwa mioyo ya watu. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Amina.

47 Katika ninii, somo hili usiku wa leo la *Makongamano*, hivi majuzi tumesikia mengi sana kuhusu makongamano, popote unapochukua gazeti karibu unaona ambapo mwanadiplomasia fulani ama afisa fulani alikuwa na kongamano mahali fulani, na—na mambo fulani yakatukia. Nasi tunashangaa, kwani makongamano ni ya nini? Kwa nini—kwa nini tunafanya makongamano? Ni ya kufanya nini? Ni ya kukusanyika pamoja, na kuhojiania mambo mbalimbali; tunapokuja kwenye kongamano, tunapaswa kuhojiana mambo pamoja.

48 Nami nafikiri hili ni moja ya Maandiko mazuri sana, wakati Mungu aliposema, "Njoo, na hebu Mimi nanyi tufanye kongamano, hebu tukutane, na kwa namna fulani tuzungumzie mambo: dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu. Iwapo tu mtakuja, tupate kusemezana."

49 Nasi tunaona usiku wa leo, kama kila mtu ajuavyo, ya kwamba sisi, kwa kweli, tunapoteza msimamo, tunapoteza msimamo kama watu. Ulimwengu unanyemelea miongoni

mwetu kwa njia fulani, unaweza kuuona, kuuhisi, na unaweza kuutambua; ulimwengu unaingia miongoni mwetu. Kwa hiyo nafikiri huu kuwa ni wakati mzuri sana kwetu kufanya kongamano, tuje tusemezane na Mungu, tuone kuna nini.

50 Nilikuwa nikisoma kitabu cha maisha ya Charles G. Finney, cha jinsi yeye akiwa wakili, naye. . .Kuna sheria zetu nyingi ambazo msingi wake ni Biblia, ambazo zilimfanya ku—kuisoma Biblia. Basi mle ndani alikuwa akisoma mahali ambapo Mungu alifanya ahadi hizi, naye akaona kanisa, wengi sana wao wakiuombea uamsho na kushindwa katika maombi yao, ni kwa sababu walikosa imani.

51 Unapomwomba Mungu chochote, mwite ashuke na uzungumze Naye, wala usiondoke mpaka upate jibu, ndipo utajua jinsi ya kufanya kazi tangu wakati huo na kuendelea.

52 Na jinsi ambavyo yeye alipitia njia rahisi kama ya kitoto, na kufanya kongamano hilo pamoja na Mungu, na kulizungumzia, naye alikuwa mmoja wa mashujaa hodari sana wa wakati huo ambao wamekuwako tangu Paulo Mtakatifu. Kwa sababu alilizungumzia pamoja na Mungu, na kupata misingi yake, na kupata mahali alipokuwa amesimama, na jinsi alivyosimama pamoja na Mungu, kisha akaendelea.

53 Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Hilo ndilo lingeweza kufanywa papa hapa kwenye uwanja huu, na ingetimiza zaidi ya makusanyiko mia tano nje yake.

Kwa hiyo, unasema, "Hebu tumwache mhubiri alifanye."

54 Hili ni jambo la kibinafsi, liko na kila mmoja wetu. Huenda mhubiri akafanya hivyo mwenyewe, huenda akaomba na aibariki nafsi yake, na kukaa alasiri yote chini ya upako wa Roho Mtakatifu apate kwenda mbele ya kusanyiko lake ametiwa mafuta, akihisi nguvu za Mungu, lakini isipokuwa kusanyiko hilo limekaa vivyo hivyo! Mnaona, inaleta tofauti. Hana budi kuliweka kusanyiko chini ya hali.

55 Lakini basi kama kusanyiko liko tayari kukutana na Roho Mtakatifu, basi nitawaambia, wenye dhambi watalia wakielekea Kalvari, kama tunaweza tu kulichukua kama mtu binafsi. Unawajibika tu kama yeyote wa hawa wahudumu. Mungu atakuweka, kama mtu binafsi, uwajibike.

56 Naye alisema, "Kama kuna dhambi yoyote, kukiweko na shaka lolote, kama kuna jambo lolote baya, njoo, hebu tulizungumzie. Hebu—hebu tuhojiane, tuone kuna nini, na dhambi zako zijapokuwa nyekundu sana," sasa *dhambi* ni kutokuamini, tunajua hilo, "ingawa umekuwa na shaka, ingawa umeshangaa ni lini utampokea Roho Mtakatifu, ama ungeponywa, ama kadhalika, ingawa mashaka yako ni mekundu kama bendera, yatakuwa meupe kama theluji." Unaona?

57 Mungu alifanya ahadi, Mungu atatimiza ahadi Yake. Naye amempa kila mmoja wetu mwaliko wa kuja, "Na tuje," mwishoni mwa Biblia ilisema, "Yeyote atakaye, na aje. Yeye asikiaye, na aseme, njoo. Yeye aliye na kiu na aje. Yeyote atakaye, na aje." Ni mwaliko.

58 Basi vipi kama ungekuwa na akili kama hiyo kwamba rais wetu wa Marekani angekuomba uende ukafanye kongamano pamoja na Khrushchev? Ingekuwa ni sifa ya jinsi gani, kwamba rais angekualika uje uzungumze naye, akifikiri ya kwamba—ya kwamba ungeweza kufanya kongamano pamoja na Khrushchev. Lakini kumbuka, si rais, bali Mungu wa Mbinguni amekupa mwaliko wa kuja kufanya kongamano pamoja Naye kwa manufaa yako.

59 Sasa makongamano ni kukutanika, na kwa kawaida, makongamano hufanywa katika wakati, katika hali ya hatari. Sasa, siku moja hapa tulikuwa na kile tunachojua kama lile Kongamano la Mabingwa Wanne, ambalo lilifanywa katika Vita vya Pili vya Dunia hapo wakati muhimu sana ulipofika. Wakati ulimwengu huru ulipofikia mwisho wa akili zao walikusanya watu wenye akili bora sana waliofikiri walikuwa nao, nao wakawakusanya pamoja, kwa sababu iliwabidi ku—kuweka pamoja yote waliyokuwa ili kuleta jawabu la jambo la kufanya.

60 Nafikiri leo ya kwamba wakati umewadia kwa Wapentekoste kuja pamoja, kuondoa tofauti zetu, na kuja pamoja kwa msingi mmoja, kwa kuwa makanisa yetu yanalegea sana. Nafikiri tunahitaji kongamano la usiku kucha na la siku nzima pamoja na Mungu, "Tufanye nini?" kwa maana kuna wakati muhimu sana.

61 Basi wakati rais wetu wa Marekani, na Bw. Churchill, na wanadiplomasia mbalimbali kutoka katika ulimwengu wote huru walipokusanyika pamoja, walifanya kongamano, nao wakalizungumzia, na kufanya uamuzi juu ya mambo fulani, na kufanya maamuzi ya jinsi ya kufanya wapate kushinda vita hivyo, ulimwengu uweze kukaa huru.

62 Ninamkumbuka mhudumu mmoja huko Louisville, Kentucky, rafiki yangu, wakati wa kongamano hilo, watu wanangojea waone matokeo yatakuwaje, ni uamuzi wa namna gani utakaofanywa, naye mhudumu huyu alikuwa, alikuwa amefungua redio yake, naye alikuwa akisikia taarifa kutoka kwenye hilo kongamano. Na—na hapo ndipo Mussolini, ama, Hitler na hao wengine walipokuwa wakifanya maendeleo makubwa sana. Naye alipokuwa akisikiliza kwa yote yaliyokuwa ndani yake, kusikia, kuona matokeo yangekuwaje, yale waliyokuwa wameamua kufanya, jamaa fulani alibisha mlangoni.

63 Ndipo akaenda mlangoni, na hapo alisimama mtu ameshika lundo la makaratasi chini ya mkono wake, mtoto fulani, nywele

ndefu chini shingoni mwake, na namna fulani ya ovaroli iliyovutwa kwenye nyonga zake kama mhuni wa kisasa, naye akasema, “Aisee, Mhubiri, wewe ni mchungaji wa kanisa hili hapa, una ushawishi mkubwa katika mji huu,” kasema, “Mimi ni—mimi ni mwandishi wa mashairi,” kasema, “Na—nakutaka ushuke uje unipe pendekezo, ili niweze kueneza mashairi yangu.”

64 Ndipo mhudumu huyu akasema, “Mwanangu, ingia tu kwa dakika moja, ninajaribu kusikia matokeo ya kongamano hili kuona kuhusu taifa letu, nione kile wameamua kufanya.” Naye akasema, “Si uje ukae chini mpaka hili litakapoisha?”

“Loo,” akasema, “hili ni muhimu kuliko kusikiliza hayo.”

65 Loo, kwa mtu, kama sisi ni Wamarekani halisi, hakuna kitu muhimu zaidi kuliko kusikia kongamano kama hilo kuona mahali tunaposimama. Hivyo ndivyo watu wanavyotenda usiku wa leo kuhusu kanisa, wanatoka hapa nje, na kukimbia huku na huku, na kuendelea na ulimwengu, wala hawana wakati wa kwenda kanisani kusikia, ama kuketi katika kongamano kusikia Injili ikihubiriwa. Loo, tunapaswa kuvutiwa na kila mkutano na kila kongamano ambapo watu wa Mungu hukutana pamoja, tunapaswa kuvutiwa nalo, kujua, ni wakati muhimu sana.

66 Ndipo wakafanya lile Kongamano la Mabingwa Wanne, naye Mungu akawapa uongozi. Halafu tulikuwa na Kongamano la Geneva, na kulikuwa na lingine lililoitwa Kongamano la Paris. Halafu Rais wetu mpendwa Dwight Eisenhower, hivi majuzi amezunguka ulimwengu wote huru, akifanya makongamano, na kadhalika.

67 Lakini mnajua, Mungu ana makongamano, pia. Na wakati kunapotokea wakati muhimu sana, dharura fulani kuu, nalo Kanisa liko katika hali ya hatari, Mungu huitisha kongamano. Na hebu turudi nyuma sasa kwa dakika chache, na kuweka mioyo yetu yote moja kwa moja kwenye Neno sasa, na kusikiliza kwa dakika chache, hebu na tuangalie baadhi ya makongamano ya Mungu. Tunaona makongamano ya ulimwengu, na tunasikia matokeo kutoka kwa hayo, sasa hebu turudi kwenye baadhi ya makongamano ya Mungu.

68 Ninataka kuanza usiku wa leo kutoka kwenye Kongamano la Edeni. Kulikuwako. . .Mungu alipomfanya mtu kwa mfano Wake, kisha akatoa ubavu ubavuni mwake na kumfanya mwanamke, akamfanyia msaidizi, na kuwaweka katika bustani ya Edeni wawe watoto Wake wapendwa.

69 Watoto Wake walipopotea, habari hizo za kutisha zilifika Mbinguni, “Watoto Wako wamepotea!” Mungu akaweka kando kila kitu kilichokuwako Mbinguni, asingemtuma Malaika kuwatafuta, asingetuma jeshi la Malaika, Mungu alikuja Mwenyewe kumtafuta mtoto Wake Mwenyewe aliyepotea, kwa sababu kulikuwa na hali ya hatari.

70 Ni picha nzuri jinsi gani kwa mtu asiyeamini katika Uungu wa Yesu Kristo! Jinsi ambavyo Mungu alidhihirishwa katika mwili katika Yesu Kristo apate kuja duniani, sio kulitumainia mikononi mwa Malaika ama mamlaka fulani ya kanisa, bali Yeye alikuja Mwenyewe, akafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, kumtafuta mtoto Wake aliyepotea.

71 Na hapo, wakati, hapana shaka, kwamba huenda Mikaeli alijitokeza pamoja na Gabrieli, na wakati u—ujumbe ulipokuja Mbinguni, "Watoto wako wamepotea, wametenda dhambi na kuondoka," Mungu hakumchukua Gabrieli, na kusema, "Shuka uende ukawatafute watoto Wangu," Yeye alikuja Mwenyewe. Ilikuwa ni kazi inayohitaji mwanamume, kazi inayomhitaji Mungu.

72 Hiyo ndiyo sababu ninaamini ya kwamba katika siku hizi tunazoishi, wanapojaribu kumfanya Yesu nabii tu... Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii, Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, Mwana wa Kiungu wa Mungu aliye hai. Yeye alikuwa ni zaidi ya mwonaji tu, ama mtu mwema, Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Mungu alishuka kumkomboa mwanadamu Mwenyewe, kama tu alivyofanya katika bustani ya Edeni.

73 Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Huo ni upendo. Mungu aliupenda sana ulimwengu, akajifanyia Mwenyewe mwili wa kukaa ndani yake, na akafanya maskani hapa pamoja nasi kutuokoa.

74 Si ajabu watu wameingia wazimu wakijaribu kuuelezea upendo wa Mungu. Kifungu hicho cha mwisho, ninaamini ndicho, cha wimbo ule maarufu, wa thamani wa "Loo, upendo wa Mungu, jinsi ulivyo tajiri na safi!"

> Na kama tungalijaza bahari kwa wino,
> Na mbingu zingalifanywa kwa karatasi za ngozi;
> Kila shina duniani liwe ni unyoya wa kuandikia,
> Na kila mtu kazi yake iwe ni ya mwandishi;
> Kuandika upendo wa Mungu Juu
> Ingeikausha bahari;
> Wala gombo lisingeweza kuenea yote,
> Ingawa limetandazwa anga hata anga.

75 Aya hiyo ya mwisho ilikutwa imeandikwa kwenye ukuta wa hospitali ya wendawazimu. Hakuna akili ingeweza kufahamu upendo alio nao Mungu kwa watu Wake. Wakati mwanawe alipopotea, Yeye alitaka kumtafuta Mwenyewe. Mama ataruka kupitia motoni kumnyakua mtoto wake mchanga wakati akiwa hatarini, baba angeruka kutoka kwenye jengo la orofa hamsini kujaribu kumnyakua mtoto wake mchanga, chochote kile, atoe uhai wake, hivyo ndivyo Mungu anavyowazia juu ya watu Wake,

Kanisa Lake, watoto Wake, wanapopotea. "Na tusemezane, asema Bwana."

76 Mungu alipojua hiyo—hiyo hali ya dharura inayotisha, nadhani ya kwanza iliyowahi kufika Mbinguni, ilikuwa ni wakati aliposikia ya kwamba watoto Wake walikuwa wamepotea, naye akaja kwa huzuni kuu, huku na huku kupitia bustanini, akiangalia chini ya kila kichaka, "Adamu! Loo, mwanangu Adamu, uko wapi?" Hapo walisimama Adamu na Hawa wakiwa wameshona majani yao ya mtini, nyuma ya kichaka, Baba akienda huku na huko, akipaza sauti, "Uko wapi? Uko wapi?"

77 Mungu yuyo huyo huenda huku na huku kwenye marefu ya kanisa usiku baada ya usiku, akipiga makelele vivyo hivyo, "Uko wapi? Uko wapi?" Naye anawakuta Adamu na Hawa vivyo hivyo, wakiwa na namna fulani ya kanuni ya imani waliyo nayo, ama madhehebu wanayo—wanayotegemea kuwaokoa, wakijificha, bado, nyuma ya theolojia fulani ya kujibunia wakati Mungu alipofanya matayarisho kwa ajili yako, wakati alipomtoa Mwanawe apate kufa badala yako. Huna budi kuzaliwa mara ya pili.

78 Kanuni za imani hazitafanya kazi, kongamano hilo lilifanyika kwenye jamii fulani; lakini kongamano la Mungu lilifanyiwa Edeni kushughulikia dhambi zako. Na kulikuwa na moja lililofanyika pale Kalvari, ambalo tutalifikia baadaye, kushughulikia dhambi zako, nayo shida ya dhambi, ugonjwa wako, na yote yatakayokupata, ninii, tayari yamechunguzwa, matayarisho yamefanywa. Jambo pekee litupasalo kufanya ni kumjia Mungu, na kulihoji, na kusema, "Bwana, si—sikukusudia kufanya hivyo." Maandalizi tayari yamefanywa kwa ajili yake.

79 Ndipo tunaona basi, wakati Mungu amewakuta wamesimama nyuma ya kichaka mahali fulani, wakitetemeka, huku wamevaa nguo zao za majani ya mtini, Mungu. . . Kama kawaida, makongamano ya ulimwengu, daima wanajaribu kufika Geneva na Uswisi, eneo la kupendeza, kwa hiyo inatia moyo, wanafanya eneo fulani, kisha wanaitisha kongamano. Nadhani Mungu, alipowakuta Adamu na Hawa wamejificha nyuma ya kichaka kule, wasingeweza kutoka, walisema, "Hatuwezi kutoka, Baba, tuko uchi."

Kasema, "Ni nani aliyewaambia, mlikuwa uchi?"

80 Ndipo wakaanza, kama tu ilivyo sikuzote, kile wanachoita jeshini, "kukwepa wajibu" kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine. Mungu akaangalia kote akaona mti, mahali fulani, mahali alipowazia pangekuwa pa kupendeza, naye akachukua ngozi, na kuzitupa huko nyuma vichakani, na kusema, "Jifunikeni na hizo, kisha mje mbele Zangu." Ndipo wakafanya kongamano, wakalizungumzia, ndipo Mungu akawafanyia maandalizi.

81 Loo, nina furaha sana kulikuwa na Kongamano la Edeni, si kutuacha tuende chini ya majani ya mtini na kitu tunachoweza kushona pamoja, lakini Mungu aliua kitu fulani kufunika dhambi zao na akatoa ahadi, kwamba kupitia Uzao wa mwanamke angekiponda kichwa cha nyoka, akitabiri yale Yeye angefanya.

82 Nina furaha sana kwa ajili ya Kongamano la Edeni, Yeye alifanya njia, maandalizi, njia ya kuondoa dhambi, alifanya njia ambayo ungeweza kurudi tena, kurudishwa katika ushirika, ambapo ulikuwa umepotea na kusimama nje mahali fulani, umelemewa, bila Mungu. Mungu alifanya maandalizi kwenye kongamano hili, naye akafanya, matayarisho tu ya muda, mpaka yale Maandalizi halisi yangetolewa kwa dhabihu ya maisha ya Kristo. Alisema ya kwamba angefanya hivyo, lakini kati ya wakati huo, ilibidi mwana-kondoo afe mpaka wakati huo, mpaka Mwana-kondoo wa Mungu atakapokuja, ambaye alikuwa atakiponda kichwa cha nyoka, na kichwa chake kukiponda kisigino, mpaka Kalvari.

83 Kongamano hilo lilifanikiwa. Loo, litamshinda Shetani, popote pale! Neno la Mungu litamshinda Shetani mahali popote, wakati wowote, kwa hali zozote. "Dhambi zako zijapokuwa nyekundu sana . . . "

84 Ulisema, "Ati hali zozote, Ndugu Branham?"

85 Hivyo ndivyo lilivyosema hasa. "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji. Jambo pekee ninalokuomba ufanye, ni kuja mahali Pangu palipoandaliwa, madhabahu." Mungu alifanya madhabahu, Kuna madhabahu, kuna mahali ambapo unakutana na Mungu. "Njoo usemezane Nami, nina mahali palipoandaliwa, na tiba kwa ajili yako."

86 Lilianzia Edeni, lile kongamano la kwanza, Yeye alifanya ma—maandalizi. Dharura ya kwanza ilipoitishwa, basi Mungu alitoa jibu na kufanya maandalizi. Lakini watu hawataki kuchukua maandalizi hayo, kwa namna fulani. Lakini kulikuwa na kongamano la kwanza Mungu alilofanya na mwanadamu katika hali ya hatari, Mungu alitoa uamuzi. Sio juu yetu kujiamulia yale tunayopaswa kufanya, Mungu huamua jambo la kufanya. Mungu ndiye aliyesema, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili," haikuwa u—ushirika wa madhehebu fulani, Mungu ndiye aliyesema hivyo.

87 Na Mungu ndiye aliyesema, "Usipozaliwa kwa maji na Roho, huwezi kuuona Ufalme wa Mbinguni." Huna budi kuzaliwa, hiyo ndiyo tiba ya Mungu, hivyo ndivyo alivyoamua wakati alipoinunua jamii ya binadamu katika Uwepo Wake. Haya basi, kama hilo si sahihi, sijui. Huo ulikuwa ndio uamuzi Wake. Damu ilikuwa ndiyo njia, si majani ya mtini, si kifuniko cha aina yoyote nyingine, bali uamuzi wa Mungu, kwenye kongamano la Mungu, kwa ajili ya watoto wa Mungu waliokuwa wamepotea,

matayarisho yalikuwa ni damu, imekuwa, daima imekuwa, na daima itakuwa.

88 Unaweza kushikilia msimamo wako juu yake, kama Ayubu wa kale juu ya sadaka ya kuteketezwa. Huenda wakakushtaki kwamba wewe ni *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*, mtakatifu anayejibingirisha ama chochote wanachotaka kusema, lakini mradi tu unasimama juu ya sadaka hiyo ya Damu, juu ya kuweka mikono yako juu ya kichwa cha Yesu Kristo, na kuungama dhambi zako, na kumkaribisha Roho Mtakatifu kwako, Naye akishuhudia kwamba Yeye amekupokea! Huo ndio uliokuwa uamuzi wa Mungu, hayo yalikuwa ndiyo maandalizi yaliyofanywa kwenye kongamano hilo la kwanza.

89 Nina furaha sana walikuwa na kongamano hilo. Lilitatua dhambi milele wakati alipofanya kongamano hilo. Katika utimilifu wa wakati, Yeye alimtuma Mwanawe, aliyefanywa kwa mfano wa mwili wenye dhambi uliochukua dhambi, akawakomboa hao waliokuwa chini ya damu ya mbuzi na kondoo, wakingojea wakati huo, na kuwapeleka katika Uwepo wa Mungu. Loo, ni jambo tukufu jinsi gani, kujua ya kwamba kongamano hilo lilifanywa. Nina furaha, najua kila Mkristo humu ndani ana furaha kwamba kongamano hilo lilifanyika. Hilo lilikuwa ni kongamano moja.

90 Basi hebu tuzungumze juu ya kongamano lingine katika hali ya hatari, nitaliita kongamano hili Ko—Kongamano la Kichaka Kilichowaka Moto. Mungu alikuwa ametoa ahadi kwa watu Wake, na wakati wa kutimizwa ulikuwa umekaribia, Naye alikuwa amemchagua mtu, nabii, kuwatoa watu Wake Misri, lakini nabii huyu alikuwa ametoroka, alikuwa amejaribu kufanya hivyo kwa uwezo wake mwenyewe.

91 Mnaona, kama tu ilivyokuwa katika Edeni, wakijaribu kutengeneza aproni ya jani la mtini tena. Musa alikuwa mtu mwerevu, angeweza kufundisha he—hekima ya ninii yake... kuwafundisha Wamisri hekima. Alikuwa mwerevu, alikuwa amefunzwa katika elimu yao yote, alikuwa mwanajeshi, na mtu mashuhuri, naye alijaribu hilo kwa akili zake, jinsi ya kuwakomboa watu kutoka chini ya utumwa wa Misri kwa akili zake. Haikufanikiwa.

92 Wala halitafanikiwa siku hizi. Mungu anayo njia iliyowekwa, Mungu anayo njia ya ukombozi wa dhambi, wala hauji kupitia kwa nguvu za kiakili, unakuja kupitia kwa Damu, na kifuniko cha Bwana Yesu.

93 Musa alijaribu majani yake ya mtini, nayo yakashindwa; yalishindwa wakati huo, yalishindwa katika Edeni, yatashindwa leo hii, yatashindwa wakati wowote, huna budi kuzaliwa mara ya pili. Huna budi kuja kwa njia ya Mungu ambapo kongamano Lake, ambapo waliamua jambo la kuwafanyia wenye dhambi, nawe huna budi kuja kwenye maandalizi hayo.

94 Musa alijaribu kama Adamu alivyofanya, akajifunika kabisa, na kusema, "Mimi ni mtu mashuhuri." Basi akamwona mmoja wa ndugu zake akidhulumiwa, akasema, "Sasa, mimi ni mtu mashuhuri, ninajua jinsi ya kufanya hili," akamwua yule Mmisri, ambalo lilikuwa ni kosa. Kwa hiyo mnaona, alijaribu njia ya majani ya mtini kama tu vile Adamu alivyofanya, na kama tu vile maelfu katika nchi hii wanavyojaribu kufanya sasa. Njia ya jani la mtini haitafanya kazi, Mungu aliihukumu kwenye lile kongamano. Haleluya! Samahani.

95 La, msiniwie radhi, msifanye hivyo. La, bwana, ninamaanisha hivyo, hiyo ni kweli. Sijarukwa na akili, ninajisikia tu vizuri. Mnaona? Kwa sababu ninajua ya kwamba kuna Njia moja tu ya kuingia Mbinguni, hiyo ni kupitia kwa Yesu Kristo, hiyo ndiyo Njia iliyowekwa na Mungu, hivyo ndivyo ifanywavyo. Roho Mtakatifu ndiye Njia, hakuna kitu kitakachopachukua mahali Pake, hakuna theolojia, hakuna kanisa, hakuna majengo makubwa, hakuna madhehebu, wala hakuna kitu kitakachopachukua mahali pa Damu ya Yesu Kristo, Njia ya Mungu, Roho Mtakatifu, kujazwa na Roho Mtakatifu. Ahadi ni kwa ajili yako, kama tu utaipokea. Mungu alifanya maandalizi kwa ajili ya yeyote atakaye. Kongamano lilifanywa, maamuzi yakafanywa.

96 Watu kote katika nyakati wamejikwaa kwenye hilo, rahisi sana, ikubali tu Damu. Huwezi kujifunika, chukua kifuniko cha Mungu. Huwezi kujifunza jinsi ya kufanya jambo hilo, hakuna kujifunza kulihusu, Mungu hufanya hivyo Mwenyewe, ni mambo ya kimbinguni. Ni kote maishani, Mungu ndiye hufunika, huwezi kufanya hivyo.

97 Na si kadiri unavyojaribu kufanya hivyo, huwezi tena kujisafisha na dhambi kwa kujiunga na makanisa na kuchukua kanuni za imani, kuliko chui angaliweza kuyaondoa madoa yake kwa kuyaramba. La, bwana. Kadiri anavyoyaramba, ndivyo yanavyozidi kuwa maangavu. Huna budi kufa kwa nafsi yako, mawazo yako mwenyewe, kujisalimisha na kumwacha Roho Mtakatifu akufunike kwa Uwepo Wake na nguvu Zake, huo ndio uamuzi wa Mungu. Hapo ndipo kongamano lilipoandaliwa, huo ndio uamuzi uliotolewa. Hivyo ndivyo. . .Hizo ndizo kanuni za Mungu.

98 Hebu tusijaribu kuwazia jambo lingine, hebu na tuchukue tu yale Yeye aliyosema juu yake, tuchukue njia ya Mungu iliyoandaliwa, jambo ndilo hilo. Lichukue, likubali, liamini. Mungu alitoa uamuzi, asingemwacha Malaika atoe uamuzi, asingemwacha Gabrieli autoe, asingemwacha Mikaeli autoe, alikuja kuutoa Mwenyewe. Haleluya! Na wakati alipofanyika mwili, akakaa kwetu, na akafa kwa ajili yetu, Yeye alifanya njia, Mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu Yeye ndiye Njia, Kweli, na Nuru. Hakuna mtu. . .

99 Yeye alinena hayo katika nyakati zote. Daima imekuwa ndiyo njia ya Mungu. Mungu hufanya hivyo Mwenyewe, ni watoto Wake Mwenyewe, hataliaminia Malaika. Na kama hataliaminia Malaika, hataliaminia kongamano, ama kundi la watu, acha wawe maaskofu, mapapa, wowote wale, jinsi walivyo wazuri, hilo huenda ni sawa, bali Yesu Kristo ndiye Njia ya Mungu iliyowekwa, hiyo ndiyo Njia aliyosema, Yeye aliamua hilo kwenye kongamano Lake, hiyo ndiyo Njia. Hiyo ndiyo hatuna budi . . .

100 Hatuna budi kuufuata mkondo Wake. Vipi kama katika UN walipokuwa wakikutana, ama wale—wale Mabingwa Wanne, na mmoja alikuwa ameondoka, na kusema, "Vema, nitalichukua *hivi*," na taifa lingine, *vile*? Wange—wangekuwa wametengana, wangeshindwa vita. Hivyo ndivyo tulivyo, Wapentekoste, hatuna budi kuungana pamoja, na kumjia Mungu kwenye misingi Yake kwa njia ya Roho Mtakatifu.

101 Mungu alikuwa ameamua nabii huyu atawakomboa watu Wake, naye nabii akafanya vile vile kabisa kama mwanawe wa kwanza alivyofanya, Adamu, akapitia njia ya majani ya mtini. Kwa hiyo haikuwa nzuri, Mungu aliihukumu. Ndipo basi, ilimbidi Mungu kuja kumtafuta. Alikuwa amekimbia huko nje, na kujiolea mke, na akapata mtoto, Gershomu, na kumwoa Sipora, na kuishi huko nje, kuhani wa Midiani, binti yake, naye alikuwa maskini mchungaji mwema wa kondoo, akiendelea vizuri, hakuna kitu kibaya.

102 Ndipo huyu hapa Mungu akaja, kama tu alivyofanya kule Edeni, kulikuwa na kitu kilichokuja mbele Zake, kiliishtua Mbingu tena, kama ilivyofanya kule Edeni, kabla ya Kongamano la Edeni, iliishtua Mbingu. Ilikuwa ni kitu gani? "Nimesikia kilio cha watu Wangu." Haleluya! "Nimesikia kuugua kwao, nami nimeona jasho lao na damu na mateso kwa wasimamizi. Nimeshuka kuja kushangaa ni kwa nini hawajatoka huko." Kwa hiyo, aliangalia nini kote, ndipo akamwona nabii Wake akikimbilia mahali fulani, njia ya majani ya mtini.

103 Hilo ndilo hasa analopata siku hizi, anamkuta mhubiri Wake akienda kwenye shule fulani kubwa kujifunza theolojia fulani, apate kupimwa na mtaalamu wa magonjwa ya akili kuona kama ana akili ya kutosha kuwa mmishenari, ama kumfanya mtu aokoke, hapo ndipo Yeye anapompata, huko nje katika hali hiyo ngumu. Loo, kile kanisa linachohitaji usiku wa leo ni kongamano lingine, kongamano lililoitwa na Mungu. Naam.

104 Kwa hiyo, Yeye alimpata. Aliangalia kote jangwani, akitafuta-tafuta kote, ninaweza kuona Nuru hiyo ikishuka katika kila mwanya mdogo, na kila mtini mdogo . . . dimbwi, kila mahali, ikizunguka ipate kujua jamaa huyu alikuwa wapi. Ndipo baada ya kitambo kidogo akamwona akitembea kwa starehe chini ya Mlima Horebu, loo, akiwa na wakati mzuri,

labda akicheza na watoto wake, na kuwa na wakati mzuri, alikuwa na maskini mke mzuri, naye alikuwa akiishi kwa raha. Basi akamkuta katika hali hiyo.

105 Kwa hiyo, Yeye akasema, “Sina budi kufanya kongamano, sina budi kumrudisha nabii huyu mtoro aurudie wito tena.” Natumaini Yeye atafanya mengi ya hayo kwenye uwanja huu. Loo, muda si muda mwajua, Yeye akachagua...Akasema, “Nitaona mahali ninapoweza kupata kichaka, sina budi kuvutia usikivu wake kwa njia fulani.” Kwa hiyo akapanda juu ya kichaka na kuketi hapo.

106 Loo, wakati Musa alipokiona kile kijiti, juu yake pamoja na ile Nguzo kubwa ya Moto imekaa pale juu ikiwaka moto, wala kile kichaka hakikuteketea, Yeye alifanya kongamano. Nakwambia, ukiwahi kutembea juu ya mchanga huo mtakatifu, kwenye moja ya makongamano ya Mungu, unatoka ukiwa mtu tofauti. Wakati wowote mara...

107 Adamu aliondoka akiwa mtu tofauti; Musa aliondoka akiwa mtu tofauti, bila shaka, aliandaliwa kwenda basi. Loo, wakati mwingine inakufanya ufanye mambo ya kipumbavu sana kwa ulimwengu wa nje. Itakufanya ufanye mambo ambayo unafikiri hungefanya, lakini kumbuka, umekuwa Uweponi mwa Mungu.

108 Na hebu niseme hili papa hapa: Hakuna mhubiri, kwa Mungu, amewahi kuchaguliwa kusimama nyuma ya dawati takatifu mpaka kwanza amekuwa na kongamano na Mungu, na kuja kwenye mchanga huo mtakatifu ambapo yeye na Mungu pekee wamesimama. Huna haki ya kufanya hivyo, huna haki, sijali una digrii ngapi za udaktari, hilo halimaanishi kiasi hicho kwa Mungu [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.], hata kidogo, huna budi kufanya kongamano. Iliwabidi kulifanya pale, Musa alikuwa nalo, kukutana na Mungu, ilimbidi kupokea maagizo yake kutoka kwa Mungu, na hapo ndipo ilipokuwa.

109 Na sasa, kuna mafundisho mengi sana mbalimbali na kadhalika siku hizi, nyoka wenye ndimi zilizojaa hila, mpaka wanaweza kuelezea mambo yote kutoka katika Biblia, wayaweke mbali katika siku nyingine. *Nyoka*, siombi msamaha kwa jambo hilo hata kidogo, hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa. Mwenye mgongo uliopakwa mafuta, anatembea akimetameta, amejipamba kabisa pamoja na nywele za kipilipili, huku amevaa suti rasmi, hivyo ndivyo ibilisi anavyoonekana. Yeye si mzee John Barleycorn, wiski ikitiririka kutoka kinywani mwake, yeye ni ibilisi aliyepambwa kabisa siku hizi, ninawaambia. Biblia ilisema ya kwamba alikuwa mjanja sana angewapoteza walio Wateule kama yamkini. Hiyo ni kweli.

110 Loo, yeye ni mwanafunzi wa Biblia, msomi. Alipokutana na Yesu, alimnukulia Andiko moja baada ya lingine tu, Yesu alisema, “Lakini *pia* imeandikwa!” Amina? Alikuwa ni jamaa kwelikweli.

111 Kwa hiyo Musa, huyo hapo, jinsi tu inavyokubidi kuwa. Haidhuru ulimi wa mwanadamu una hila jinsi gani, haidhuru wanajaribu kulielezea vinginevyo jinsi gani, kama umewahi kuwa upande wa nyuma ya jangwa, kama umewahi kuitwa katika Uwepo wa Mungu, na kusimama pale, na kuzungumza Naye, na kuhisi nguvu Zake zikiingia ndani yako, kama vile ile Nuru ilivyokuwa ikitoka kwenye kile kichaka juu ya Musa, na kujua ya kwamba umezungumza na Mungu ana kwa ana, pepo wote ulimwenguni wasingeweza kamwe kukuelezea hilo vinginevyo. La, bwana. Hapo ndipo mahali ulipokutana na Mungu.

112 Shetani hawezi kufanya jambo lingine lolote, kwa sababu ni mahali palipotiwa nanga nafsini mwako, hata hakuna kitu kingine kingeweza kuchukua mahali pake. Umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, nawe umezaliwa mara ya pili. Uko kwenye maeneo hayo matakatifu, hakuna mtu, ibilisi hawezi kuuweka mguu wake mchafu karibu hapo. Anaweza kueleza Maandiko, na kusema yalikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine, na *hili* kwa ajili ya siku nyingine, na *lile* kwa ajili ya siku nyingine. Hiyo haitaninii. . . Lakini inapofikia kumjua Mungu, umekutana Naye ana kwa ana, nawe unajua unachozungumzia.

113 Sasa, hilo ndilo Musa hakuwa amefanya bado, mnaona. Alikuwa na theolojia yote, lakini alichukua njia ya majani ya mtini, mnaona, lakini sasa, kama tu vile Adamu alivyofanya, bali alitaka kuwa na hekima, alitaka kujua jambo fulani. Kumbukeni, hiyo ilikuwa ni mbinu ya Shetani, "Utakuwa na hekima na kujua. Hujui sasa, lakini nitakupa hekima kama ukienda katika shule yangu." Atakupa mengi, yote utakayo.

114 Lakini inakubidi tu kujua jambo moja: Yesu Kristo alikufa ili kuwaokoa wenye dhambi. Na uje Kwake, mkubali, tubu. Kweli kabisa. Rahisi tu, kasema, "Ingawa mpumbavu hapaswi kukosea katika njia hiyo," Isaya alisema, Mungu alililifanya rahisi sana. Nina furaha alifanya hivyo, la sivyo kamwe nisingeweza kulielewa. Kwa hiyo Yeye alililifanya tu rahisi, kusudi sote tuweze kuelewa. Hivyo ndivyo Mungu alivyolifanya.

115 Sasa, na wakati alipozungumza na Musa kwenye kichaka kilichowaka moto, naye Musa akapata kumwona Mungu kwa karibu. Alifikia mahali ambapo hakuwa amewahi kuwapo awali, kitu fulani kikatia nanga ndani yake, imani ikainuka ndani yake. Ambapo asingeweza kufanya hivyo kwa jeshi, hapa alikuwa anaenda kufanya hivyo mwenyewe, yeye na Mungu, kwa maskini fimbo iliyopinda. Mnaona? Alifanya kongamano.

116 Alishuka moja kwa moja Misri na kufanya yale hasa Mungu aliyomwambia afanye, akafanya ishara na maajabu, na kila kitu kingine. Naye Mungu akaacha nyakati ngumu zije zimpige makonde, na kumwangusha chini, kumgeuza, lakini aliamka

moja kwa moja tena, na kusema, "Ninajua ni kweli. Nilikutana na Mungu, nami nitawatoa huko."

117 Huku Yane na Yambre wangeweza kusimama na kutupa fimbo zao chini, zikageuka kuwa nyoka, wangeweza kufanya mambo yale yale, kama tu vile karibu mwanamizimu anavyoweza kufanya siku hizi, "kuwapoteza walio Wateule kama yamkini," kuita umati mkubwa, na kuwa na *ninii* kubwa, na kila kitu, hilo halilikomeshi hata kidogo.

118 Kama umewahi kuwa Uweponi mwa Mungu, unajua mahali unaposimama. Unajua Baba yako ni Nani, unajua ulizaliwa kutoka wapi. Kama mtu hana zaidi ya kupeana mkono, na jina kwenye kitabu, na barua katika kanisa fulani, hajui baba yake alikuwa ni nani. Kweli.

119 Kama kuna kitu chochote ninachohurumia, ni nyumbu. Usininii. . . Sasa, Mungu aliumba vitu vyote, bali Yeye hakuumba nyumbu. La, bwana. Kama vile Booth-Clibborn alivyozoea kusema, "Yeye hakumwumba." La. Mnajua, hicho ni kile alichofanya mwanadamu, yeye—yeye—yeye alimzalisha farasi na punda jike, hilo ndilo lililosababisha nyumbu. Hawezi kujizalisha tena, hawezi kujizaa tena, hiyo ni kweli, hana budi kukaa papo hapo alipo. Na kama kuliwahi kuwa na baradhuli, ni nyumbu. Hiyo ni kweli. Mbona, unaweza kuketi na kumpigia tu makelele, na kumpigia mayowe kadiri utakavyo, atayanyosha hayo masikio makubwa na kukuangalia tu.

120 Hiyo ni kusema, nimeona wengi sana wao mikutanoni, unazungumza juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, wanaamka na kwenda nyumbani, kama nyumbu. Hiyo ni kweli kabisa. Hawajui baba yao alikuwa ni nani, wanasimama tu hapo na kuangalia, na, "*Hoo*, *hoo!* Siku za miujiza zimepita. *Hoo!* Hakuna kitu kama hicho. *Hoo*, *hoo!*"

121 Sasa, farasi hayuko hivyo, yeye ni mpole na mzuri, anakuja, anaweka shingo yake juu ya bega lako na kuguna, naye ni mpole, bali si nyumbu wa kale asiye na maarifa. Sasa, yeye hajui baba alikuwa ni nani, mama yake alikuwa ni nani, hawezi kujizalisha tena, hawezi kujizaa, yeye ni ninii tu, yeye ni chotara.

122 Hiyo ndiyo shida ya watu wengi *wanaojiita* Wakristo siku hizi, waliochanganywa mbegu na ulimwengu. Si ajabu kamwe huwezi kutulia, "mwenye nia mbili, kamwe huwezi kuufikia ujuzi wa ile kweli." Mwanadamu hana budi kumjua Mungu kwa kuzaliwa upya, na kuzaliwa na kujazwa na Roho Mtakatifu, wasimame katika njia hizo—hizo pale, ambapo Musa alisimama, wasimame katika Uwepo wa Mungu na kufanya kongamano, hapo ndipo Mungu alipomwitia mwanadamu. Bila shaka.

123 Musa anashuka moja kwa moja kwenda Misri, na haidhuru ni jambo gani gumu linalokuja, Wamisri wote, na kadhalika wangeweza kutenda, na kufanya, na kuiga, hilo halikumzuia

Musa, alizidi kusonga mbele, kwa sababu alikuwa amefanya kongamano na Mungu.

124 Huenda kukawa na washika nyoka, na loo, sininii... watembea motoni, na kadhalika waliojitokeza ulimwenguni, lakini mtu aliyepata kumpokea Roho Mtakatifu anajua mahali hasa anaposimama kama amewahi kufanya kongamano na kuzungumza na Mungu, amezaliwa, mambo hayo hayamtikisi, bila shaka hayamtikisi. Anajua Yule anayemwamini, anajua Baba yake ni Nani.

125 Je, si ni vizuri sana kumtazama farasi ukoo safi? Unarudi kwenye ukoo wake, unajua baba yake alikuwa ni nani, babu yake alikuwa ni nani, babu wa babu yake alikuwa ni nani, unarudi tu nyuma, yeye ana ukoo safi. Nawaambia, tuna Wakristo wengi sana waliotawanyika wasio na ukoo safi.

126 Wasema, "Nilikuwa Mmethodisti juma lililopita, Mbaptisti juma moja kabla ya lililopita, na Mpresbiteri kabla ya hapo, na Mpentekoste kabla ya hapo, na..." Loo, jamani, hawana ukoo wowote safi kamwe.

127 Lakini mtu aliyemjia Mungu, na kusimama Uweponi mwa Mungu, na kuikubali neema ya Mungu na wokovu Wake, amezaliwa mara ya pili, na kujazwa na Roho Mtakatifu, yeye ni mwana wa Mungu. Haleluya! Pepo wote katika kuzimu hawawezi kumtikisa amwondoshe mle, anajua mahali alipo, anajua Baba yake ni Nani, anajua zinakotoka nguvu zake, anajua Yeye aliyemwamini, anajua Yeye ni Mungu! Bila shaka. Anajua Neno Lake, anadumu nalo, anamwamini Mungu, anakula—anakula Chakula cha watoto, anakula Chakula cha kondoo. Wengi kupita kiasi wanakula magugu siku hizi badala ya Chakula cha kondoo, wakifa kwa njaa.

128 Tunachohitaji leo ni Roho Mtakatifu kurudi kuwalisha watoto, chini karibu na malisho ya kijani kibichi yenye kivuli na maji matulivu. Bila shaka. Amani ya Mungu, kama mto unaotiririka kupitia nafsini mwetu, tukijua ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia uzimani, ya kwamba sisi ni viumbe vipya katika Kristo Yesu.

129 Vema, alifanya yale hasa Mungu aliyomwambia afanye. Alipokuwa akienda zake, alikutana na upinzani. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hiyo ni kweli. Utakutana nao moja kwa moja kwenye wajibu, ukimshuhudia Mungu, ukifanya jambo lifaalo, utagonga—utagonga mwamba. Bahari ya Shamu ilikuwako.

130 Sasa, tutazungumza juu ya kongamano lingine, tutaliita hili Kongamano la Bahari ya Shamu. Moja kwa moja kwenye wajibu, ambapo Musa aligonga mwamba, kulikuwako na Bahari ya Shamu mbele zake, jeshi la Farao likija, milima na majangwa kila upande, hakuna njia ya kuepukia, ilivyoonekana.

131 Sasa, tunapoingia kwenye wajibu, na kugonga kitu kama hicho, ni wakati wa kuitisha kongamano. Nafikiri hapo ndipo kanisa la Kipentekoste limefikia usiku wa leo, katika mstari wa kujaribu kushikilia kitu sahihi, kuna mahali ambapo tumegonga mwamba mahali fulani, ni wakati wa kufanya Kongamano la Bahari ya Shamu. Hatuna budi kuvuka kwenda ufukoni, Mungu alitoa ahadi, hatuna budi kuvuka.

132 Nao wakafikia kwenye lile Kongamano la Bahari ya Shamu. Musa alifanya nini? Kamwe hakufadhaika na kusisimkwa kabisa, kasema, "Vema, nitaenda kujiunga na hili *lingine*, ama nije kwenye kundi hili *lingine*, ama nitakubaliana na Farao, labda nilikosea, ninapaswa kufanya kongamano la amani pamoja naye." La, bwana. Alikuwa kwenye wajibu, naye alikaa kwenye wajibu wake.

133 Lakini jambo alilofanya lilikuwa ni kwenda na kujichagulia jiwe kubwa mahali fulani, ningewazia, naye akaingia nyuma ya jiwe hili kubwa, akakaa pale kwa muda, na kusema, "Bwana Mungu, niko kwenye wajibu, nimefanya kila kitu ulichoniambia nifanye, sasa ninakabiliwa na jambo fulani."

134 Mnajua uamuzi uliofanywa? Ninawazia ninawaona Malaika wameketi juu ya kila mwamba, kote namna *hii*. Huyo hapo Musa moja kwa moja kule chini, huyo hapo Mungu, amesimama hapo akimsikiliza. Kasema, "Niko moja kwa moja kazini, na kuna jeshi la Farao linalokuja, nami ninajua ya kwamba Wewe uko hapa mahali fulani, maana ulikuwa ukiangaza kule juu katika ile Nguzo ya Moto, kwa hiyo Wewe uko hapa mahali fulani."

135 Na Malaika wote wanakusanyika, nao Malaika wakamwangalia Mungu, waone kile ungesema. Akamwambia mmoja wa wale Malaika, "Nenda ukaseme naye, kisha umwambie asimame, asonge mbele." Amina.

136 Kamwe humsikii Mungu akisema rudi nyuma. Kamwe usirudi nyuma, songa mbele mradi tu uko kwenye wajibu. Tume—tumepokea kuhesabiwa haki, hatujui kutakaswa kunamaanisha nini, ni wajibu, songa mbele. Kama umetakaswa, hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu, ni wajibu, songa mbele. Kama wewe ni mgonjwa na huwezi kupata afya, umefanya yote uliyoambiwa na daktari ufanye, na bado huwezi kupona, wajibu wako ni kusonga mbele. "Songa mbele, nena na hao watu, kisha uende mbele." Endelea tu kusonga mbele.

137 Musa akanena na watu, akasema, "Jitulizeni." Akaokota fimbo yake, akaanza kutembea kuelekea Bahari ya Shamu, ikaondoka tu.

138 Hiyo ndiyo maana ya kongamano, kusukuma upinzani. Amina. Ndipo mnaweza kuwa na ibada ya uponyaji, mtakapowatoa akina Tomaso wote, na wenye shaka wote, na *haya* yote, *yale*, na *mengineyo*, na za kawaida zote, mtoe

majani yote ya mtini, na kuyavua wakawa tupu, uwafunike kwa Damu, ndipo wao ni wana na binti za Mungu.

139 Kama tu vile nimesema mara nyingi, ni kama tu majira ya kuchipua sasa, maskini mama ndege atatoka, na—naye atajitengenezea kiota kikubwa, na kukijaza manyoya, kukitayarisha kwa ajili ya makinda wa ndege. Naye angeweza kutaga kiota kizima cha mayai, lakini kama hajawa na mwenziwe, mayai hayo yatakaa papo hapo na kuoza, kamwe hayataanguliwa, hayajarutubishwa.

140 Na hivyo ndivyo washiriki wengi wa kanisa walivyo, wanakuja kanisani, nanyi mnawapigapiga mgongoni, wanavaa vizuri, wanatoa sadaka vizuri kanisani, na kadhalika, na karibu wamshughulikie mhubiri, wakati wote yuko huko nje kwenye namna fulani ya mkutano wa kijamii, ama kitu kama hicho, mambo haya yote ya namna hii, lakini kama hawajawa pamoja na Mwenzi, Yesu Kristo, ni kama tu kiota kilichojaa mayai yaliyooza, afadhali utupilie mbali kitu hicho na uanze upya.

141 Tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na kongamano na Mungu tupate kukutana na Mwenzi wetu, Yesu Kristo. Yeye ndiye Mwenzi wa Kanisa, Yeye ndiye Bwana-arusi wa Bibi-arusi. Kutana Naye, upate kujazwa na Roho Wake, Bwana-arusi.

142 Kwa hiyo Musa akafanya Kongamano hili la Bahari ya Shamu, akapokea amri, na akasonga mbele. Kulikuwako na kongamano lingine ninalopenda, nina dazani moja ya hayo iliyoandikwa hapa chini, bali nataka kuharakisha niendee moja sasa.

143 Kulikuwa na Kongamano la Gethsemane wakati mmoja, ambapo Yesu kama mwanadamu. . . Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu, Mwana wa Mungu aliyeumbwa, Mungu alimtia uvuli Mariamu, na kuumba Seli ya Damu ndani yake iliyomzaa Mwana, Kristo Yesu, naye Mungu akashuka na kukaa ndani Yake, ndani Yake mlikuwamo utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.

144 Timotheo wa Kwanza 3:16 ilisema, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu, kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na Malaika," na kadhalika, "akapokelewa juu Mbinguni." Ee Mungu! Si nabii, Mungu aliyefanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, Huyo hapo, Imanueli. Roho Mtakatifu alimwita Imanueli, "Mungu pamoja nasi." Na sasa ni Mungu ndani yetu, Roho yeye yule.

145 Tunampokea kwa sehemu, kipimo, Yeye alimpokea bila sehemu wala kipimo, "Ndani Yake mlikuwamo utimilifu wa Mungu." Yote aliyokuwa Mungu Yeye aliyamimina ndani ya Kristo, naye Kristo wote alimwagwa juu ya Kanisa. Amina. "Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Loo,

jamani, inapofikia siku hiyo! Sasa, tunaendelea, tuna maagizo, endelea tu kusonga.

146 Gethsemane ilifikia mahali fulani. Angeweza kuwa Mfalme, isingemlazimu kufa kamwe. Lakini je, atafaulu? Alisema katika kongamano hilo, wakati malaika wamesimama kila upande kuona uamuzi Wake ungekuwa nini, wakati walipokuwa—walipokuwa wanamtemea mate usoni Mwake, na wakienda kumfanyia kila kitu, Yeye alisema, "Si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke." Loo, laiti tungaliweza kufanya hivyo!

147 Unasema, "Vema, sasa angalia, Ndugu Branham, kama nikimpokea Roho Mtakatifu, mama yangu, baba yangu, bosi wangu, nanii wangu . . . "

148 Lakini vipi kuhusu Bwana wako? Jambo ndilo hilo. Ata—atasemaje juu yake kama ukimkataa?

"Vema, kanisa langu . . . "

149 Vema, najua huenda hilo likawa gumu, lakini vipi kuhusu Bwana wenu? Unaona, kanisa lako haliwezi kukuokoa, inahitaji Bwana. Unaona? Unaona, huna budi kufanya uamuzi huo, huna budi kufikia wakati huo, kila mtu hana budi kuufikia. "Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa na Mungu," kurudiwa, kurudiwa kuona kama yeye ni mwana wa kweli wa Mungu.

150 Hapo, Yeye alikuwa amesimama pale, Naye akasema, "Si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke."

151 Halafu kulikuwa na kongamano lingine, ninalotaka kuzungumzia mara moja, na hilo lilikuwa ni Kongamano la Pentekoste. Loo, ndugu, jinsi tunavyohitaji lingine la hayo! Idadi ya watu hao ilikuwa mia na ishirini. Kwa matunda yote ya huduma Yake, kwa mikutano yote mikuu aliyokuwa amefanya, makumi ya maelfu aliyokuwa amewaponya, alikuwa na mia na ishirini waliokuwa tayari kusimama na Yeye kutoka katika taifa. Walipokuwa wameona kila kitu ambacho kingeweza kufanywa, kazi kuu za kila namna, na kadhalika, alikuwa na mia na ishirini walioshikamana Naye.

152 Nao walikuwa wamemsikia Mungu akisema hivi: "Lakini mtapokea nguvu, baada ya haya, Roho Mtakatifu akiisha kuja juu yenu. Ndipo mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi, na Samaria, na ulimwenguni kote. Mnapaswa kwenda ulimwenguni kote na—na kuanzisha Kanisa, kuimarisha imani miongoni mwa watu. Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.

153 "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Kwa Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watashika nyoka, kunywa vitu vya kufisha, wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Loo, jamani!

154 "Lakini ngojeni kidogo, msiende wakati bado, kutakuwa na kongamano litakalofanywa, nitawapasha habari. Nendeni tu Yerusalemu, mkangojee huko juu. Fungueni redio yenu mngojee taarifa."

155 Mtaliendeshaje Kanisa hili? Ninasema hili kwa heshima, kwa uchaji, kwa upendo, na kwa heshima kwa kila mwanamume, kila mwanamke katika kila dhehebu, "Tunapanda kwenda kule tuone kama tutakuwa na madhehebu au la. Je, tutaliendesha kwa lundo la kanuni za imani? Je, tutaliendesha *hivi*, ama *vile*? Tutafanyaje jambo hilo? Vema, hebu tupande juu, tungoje mpaka hilo kongamano litakapokwisha. Yesu amepanda kwenda kwa Baba, tutaona kitakachorudi katika dakika chache." Kwa hiyo wakangojea.

"Utasubiri muda gani?"

"Mpaka lile kongamano litakapokwisha."

"Siku ngapi? Mbili?"

"La, mpaka tu litakapokwisha, mpaka."

"Mpaka nini?"

"Mpaka lile kongamano litakapokwisha."

156 Vema. Baada ya kongamano kwisha, wote walikuwa huko juu wakingojea, hawa mia na ishirini wakingojea kuona kitakachotukia, jinsi ambavyo hawana budi kuliendesha Kanisa, kile kinachowabidi kufanya. Je, wanapaswa kuwa na kitabu kikubwa mno na kubeba majina yote? Au wanapaswa . . .? Inawapasa kufanya nini? Sasa, watapata malimbuko yake.

157 Walipokuwa wameketi pamoja, akaja kuhani mmoja akiwa na Ekaristi takatifu katika kibweta, kasema, "Toa ulimi wako." Hilo si linasikika la kipumbavu?

158 Huyu hapa anakuja mmoja akiwa na kichupa kidogo cha maji ya chumvi, na kusema, "Hatuna budi . . . " Mwajua. Hakuna kitu kama . . .

159 Ama, huyu hapa mhubiri Mprotestanti anakuja barabarani, Dk. *Nanii*, kasema, "Nipe mkono wa kuume wa ushirika, nasi tuandike jina lako kwenye kitabu."

160 Hilo si—hilo si lingesikika kama Pentekoste? Hivyo ndivyo tunavyojaribu kulifanikisha. Ni kitu gani? Msinikasirikie. Mnaona? Yangali ni majani ya mtini, kabisa, ni majani ya mtini.

161 Walikuwa wakingojea katika kongamano hilo kuona kile ambacho kingetukia kwa Kanisa, ndipo kasema, "Kukaja, kwa ghafla, sauti kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi," matokeo yalikuwa yakirudi, "ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Ndimi zilizogawanyika zikawakalia, kama moto. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha zingine, kama Roho alivyowajalia kunena.

162 "Palikuwa na Wayahudi wakikaa Yerusalemu, watu watauwa, kutoka kila taifa chini ya mbingu. Hili likasikika kote, wakakusanyika na wakafadhaika, kwa sababu walimsikia kila mtu akinena kwa lugha yake mwenyewe aliyozaliwa nayo.

"Wengine walikuwa—walikuwa wakidhihaki, wakifanya mzaha, kasema, 'Hawa wamejaa mvinyo mpya.'"

163 Mwangalie msemaji mkuu sasa, baada ya kupata taarifa kutoka kwenye kongamano, alisema, "Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu: Watu hawa hawajalewa, kama mnavyodhania, kwa kuwa ni saa tatu tu ya mchana. Vilabu vya pombe havijafunguliwa bado." Naam, bwana. "Hii ni saa tatu mchana. Lakini jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, 'Na itakuwa katika siku ya mwisho,' asema Mungu, 'nitamwaga Roho Yangu juu a wote wenye mwili.'" Hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuendeshwa. Loo!

164 "Wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na wale watu wengine, 'Ndugu zetu, tutendeje?'

165 "Yeye akasema, "Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi ya Kanisa ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

166 Hayo yalikuwa matokeo ya kongamano la Mungu pamoja na Mwanawe Mbinguni. Hivyo ndivyo Kanisa lilivyowekwa katika utaratibu. Haleluya! Roho Mtakatifu alikuwa aliongoze Kanisa, sio maaskofu, na maaskofu wakuu, na mapapa, na baba, na babu, lakini lilikuwa liongozwe na Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo linavyopaswa kuwa, hivyo ndivyo kongamano la Mungu. . . hivyo ndivyo matokeo yalivyokuwa. Hivyo ndivyo ilivyopaswa kuwa. Kitu kingine chochote nje ya hayo ni lundo la majani ya mtini, wala hakifai kitu. Toka nyuma yao, na halafu uyararulie mbali kutoka kwako, ujifanye tupu mbele za Mungu. Uwe na . . . Njoo ukapatanishwe.

167 "Njoni mfanye kongamano pamoja Nami, hebu tulizungumzie, ingawa kutokuamini kwako kumekuwa kwekundu sana, nitakufanya kweupe kama theluji." Atakuthibitishia. Kongamano, Kongamano la Kipentekoste.

168 Nina kongamano lingine, na kisha tutafunga, tuna mengi sana hapa, lakini nina moja zaidi sina budi kulifikia. Ndipo baada ya yapata siku nne ama tano baada ya Pentekoste, Petro na Yohana walikuwa tu wanaenda hekaluni siku moja kuomba. Kulikuwako na maskini mtu aliyelemaa, kwa namna fulani mlemavu tangu tumboni mwa mama yake, mwenye umri wa kama miaka arobaini, naye akatikisa-tikisa maskini kikombe chake, alitaka kitu.

169 Nami ninaweza kuthibitisha ya kwamba Petro na Yohana walikuwa wahubiri wa Kipentekoste, walisema, “Sina fedha wala dhahabu.” Hiyo ni kweli, naam, bwana. Wakasema, “Sina fedha wala dhahabu, Sina pesa zozote, lakini nilicho nacho, nitakupa.”

170 Mungu, nijalie kuwa na *hicho*, sitaki pesa, nataka *hicho*. “Nilicho nacho, ninamwamini Yeye, nimejazwa na Roho Wake, Yeye anakaa ndani ya moyo wangu. Anaishi ndani yangu kama tu vile alivyoishi katika Kristo, sio sana, bali Yeye ni . . . Mimi ni mwanawe. Nilicho nacho, nitakupa: Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama utembee.” Whiu! Loo, jamani!

171 Ilibidi kongamano lifanyike. Walifanya nini? Kanisa kuu la Sanhedrin, madhehebu makubwa yalisema, “Tutakomesha upuuzi huu. Hakuna mmoja wa uponyaji huu wa Kiungu hapa, siku za miujiza zimepita.” Hakika, waliliamini. “Huenda ilikuwa hivyo huko nyuma katika siku za Musa.”

172 Lakini Musa alisema . . . Katika siku za Musa ilikuwa huko nyuma kabisa mahali pengine, daima wanayaweka katika wakati uliopita, ama mbali mahali fulani katika siku za usoni.

173 Nilimsikia mtu fulani akisema wakati mmoja ya kwamba uponyaji wa Kiungu utakuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Vema, una mwili uliotukuzwa wakati huo, kwa hiyo unahitaji uponyaji wowote wa Kiungu kwa nini? Ni ibilisi akijaribu kukuweka kando katika kitu fulani huko ng’ambo, Utawala fulani wa Miaka Elfu utakuwa *kitu fulani*, ninyi, sasa hivi, ni wana na binti za Mungu. Amina. Kama theolojia yako ya kujibunia ilikupa marupurupu kidogo, baridi na kukwambia ungoje, wewe endelea, bali nina mlo kamili wa chakula cha kutwa cha Roho Mtakatifu. Vema, Msifu Mungu, hiyo ni kweli.

174 Wanataka kukwambia usimame huku nje, na kula maganda, ama kutafuna mifupa, na kukwambia ya kwamba kuku wote wamekwisha tangu miaka mingi iliyopita, usiamini hilo, Mungu ana mlo kamili kwa ajili ya mtu mzima, aliye na imani kamili katika Mwana wa Mungu na analiamini, na atafuata maagizo. Menyu inasema: “Kila atakaye, na aje. Nayo ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Haleluya! Ninaamini ningeweza kucheza kitu hicho sasa hivi, kweli ninaamini.

175 Hiyo ni kweli, ndugu. Roho Mtakatifu yeye yule pamoja na ishara zile zile, maajabu yale yale, nguvu zile zile, naam, bwana, Roho Mtakatifu wa Mungu! Loo, najua inakufanya usikike mpumbavu kwa ulimwengu, lakini unajali nini kuhusu ulimwengu?

176 Ninawazia kama, kama alivyofanya Daudi, alijazwa sana na utukufu wa Mungu, alipoona sanduku hilo likija, alikimbia

huko nje na kugonganisha miguu yake juu sana hewani, akaanza kucheza dansi kote kote.

177 Na maskini mke wake, mwenye kiburi, kama wa kimadhehebu, akaangalia nje ya dirisha, naye akasema, "Loo, jinsi anavyoniaibisha!" Kwa hiyo usiku huo wakati Daudi alipokuja nyumbani, alisema, "Daudi, ulikuwa unafanya nini huko nje," kutenda kama mpumbavu, kwa maneno mengine, "ukicheza dansi huku na huku, kupiga mayowe, ukirusha-rusha miguu yako juu kabisa hewani?"

Akasema, "Nilikuwa nikicheza na kushangilia mbele za Bwana."

178 Mungu aliangalia chini kutoka Mbinguni, akasema, "Daudi, wewe ni mtu anayeupendeza moyo Wangu." Hakika.

179 Ndipo mke wake akajawa na kiburi juu yake, ndipo ikawaje? Alikuwa tasa maishani mwake mwote, Mungu aliweka laana juu yake. "Amelaaniwa mtu yeyote atakayemgusa mtiwa mafuta wa Mungu, usimguse mtiwa mafuta Wangu." Hiyo ni kweli. "Kwa maana yakufaa ufungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari, kuliko hata kumkosesha mmojawapo," hiyo ni kweli, "wa wadogo hawa wanaoniamini Mimi. Na ishara hizi zitafuatana na wadogo hao wanaoniamini Mimi."

180 Hilo ndilo linaloleta tofauti, hilo ndilo linalokwambia kama umekuwa kwenye kongamano au la, hiyo ni kweli, "Ishara hizi zitafuatana na hao." Loo, Yeye ni mwema sana. Hakuna mahali pa kusimamia, sivyo? Hebu tumalize kongamano hili.

181 Wakawapeleka kule juu, na kusema, "Vema, geuza migongo yao, tutawapiga mijeledi kidogo." Wakasema, "Hebu niwaambie jambo moja sasa hivi, msihubiri tena uponyaji wa Kiungu katika Jina la Yesu."

182 Petro akasema, "Vema, kuna jambo moja tu," wakawaachilia, kasema, "Yohana, hebu twende tukafanye kongamano."

183 Wakapanda juu, wakawachukua wengine wao, wakakutanika. Mmoja akinena, "Vema, Bwana alifanya *hivi-na-hivi* hapa chini." Wakati kundi hilo la Kipentekoste lilipokusanyika pamoja, shuhuda zilikuwa zikitoka kila mahali, yale Mungu alikuwa amefanya.

Kasema, "Hebu tufanye kongamano."

184 Kwa hiyo wote wakakusanyika pamoja, nao wakapiga magoti, kama tunavyopaswa kufanya usiku wa leo, hiyo ni kweli, wote wapige magoti, na kusema, "Bwana, mbona mataifa wakafanya ghasia, na watu wanatafakari ubatili?" Kasema, "Kweli, dhidi ya Mtoto Wako Mtakatifu, Yesu." Kisha kasema, "Ee Bwana, tujalie nguvu na ujasiri wa kunyosha mikono Yake mitakatifu kuwaponya wagonjwa."

185 Walikuwa wakifanya kongamano, nao walikuwa wanangojea matokeo. Na yapata tu wakati huo, matokeo yakarudi kutoka Mbinguni, ndipo yaliporudi, nguvu zilijaa mahali pale na kulitikisa lile jengo ambamo walikuwa wamekusanyika pamoja. Nao wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri, na kuhubiri uponyaji wa Kiungu mpaka wa mwisho kati yao alipokufa.

186 Makongamano, loo, kunayo mengi. Dharura. Walikuwa wakitaka kufanya nini? Walikatazwa na sheria kufanya hivyo. "Tutamsikiliza nani, sheria ama Mungu?" Petro akasema papo hapo katikati yao wote, walisema, "Msihubiri tena katika Jina la Yesu."

187 Akasema, "Nimsikilize nani, wewe ama Mungu?" Hiyo ni kweli.

188 Nao walisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa, hakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe, na hata hivyo, aliachiwa funguo za Ufalme. Jinsi Mungu anavyofanya mambo! Kama hilo si zuri sana! Naam, bwana. Mungu alimpa funguo na kumwambia, "Utakalofunga duniani, nitalifunga Mbinguni," na hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe. La, bwana.

189 Ni mtu wa namna gani kumwachia hizo funguo! Lakini yeye. . .Lakini wao wakamzingatia, wakatambua kwamba alikuwa pamoja na Yesu. Hilo ndilo wanalotaka kujua siku hizi. Alikuwa kwenye kongamano wakati mmoja pamoja na Yesu, naye alikuwa amepokea kitu fulani.

190 Sasa, ndugu, ingekuwa . . .? Hebu niwe na kongamano moja dogo tu, kabla sijafunga. Angalieni, kuna kongamano lingine linalokuja, huenda hukuhudhuria la Geneva, wala na mimi sikuhudhuria; huenda hukuhudhuria lile—lile la Mabingwa Wanne, ama la Paris, ama lolote la makongamano hayo mengine; na huenda hata hujawahi kuhudhuria kongamano lolote pamoja na Mungu, hapa, lakini hebu nikwambie jambo fulani, hili, rafiki yangu, kuna moja utakalohudhuria, na hilo ni hili: Hukumu.

191 Wote watakuwepo, utahudhuria kongamano hilo. Na kuna kitu kimoja tu ambacho Mungu atatambua, hicho ni Damu ya Mwanawe Mwenyewe. Je, umefunikwa Nayo, rafiki? Loo, utalihudhuria, sijali wewe ni nani, utasimama Mbele za Mungu, na hiyo itaamua kikomo chako cha Milele cha hukumu Yake. "Na nitakapoiona ile Damu," wala si kitu kingine, bali ile Damu, "nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu."

192 Ni watu wangapi hapa ambao hawajawahi kuhudhuria Kongamano la Mungu la Roho Mtakatifu na kujazwa Naye? Hebu tuone mikono yenu, ambao bado hawajajazwa na Roho Mtakatifu, inueni mikono yenu. Ni wangapi humu jengoni hawajawahi kumpokea Roho Mtakatifu?

193 Kuna mwenye dhambi hapa ambaye hajawahi kufanya kongamano na Mungu kamwe? Inueni mikono yenu, na kusema,

"Sijawahi kufanya kongamano na Mungu, mi—mimi ni mwenye dhambi." Sasa, kuwa mwaminifu, kuwa mwaminifu. "Sijawahi kufanya kongamano."

194 Hebu niseme tu jambo hili kabla ya kufunga, ni—nimeshawishika kufanya hivyo sasa hivi: Kama mhudumu, ninakiri, ya kwamba daima iliniogopesha nilipowazia juu ya kifo. Itakuwaje kwangu kati ya sasa, nitakapokufa, na Kuja kwa Bwana Yesu? Nikikutana na marafiki zangu Mbinguni, wangekuwa ni maskini roho ndogondogo.

195 Nilidhani roho ingenitoka, na tuseme kungekuwako, ningemwona Ndugu Sullivan, nami ningesema, "Huyo hapana shaka ni Ndugu Sullivan, maskini roho hiyo. Siwezi kushika mkono wake, umeozea kaburini, si—siwezi kumwangalia kwa macho, maana macho yake yamekwisha, yangu yamekwisha, pia," mnaona, "Si—si—siwezi kumgusa, kwa sababu yeye ni roho tu." Ilinitia wasiwasi, na—nataka kuzungumza naye.

196 Hivi majuzi asubuhi, yapata Jumapili tatu asubuhi zilizopita, nilikuwa nimelala kitandani, nami nikaamka yapata saa moja, tunaenda kanisani saa tatu na nusu, basi nikainuka, nikamwangalia mke wangu, naye alikuwa amelala usingizi mzito. Nilianza tu kulichunguza jambo hilo.

197 Nikaendelea kusikia Kitu fulani kikisema, "Kaza mwendo, endelea tu kukaza mwendo."

198 Nikasema, "Vema, nina umri wa miaka hamsini, si—sina budi kumfanyia Bwana jambo fulani, sijafanya lolote bado. Naye akaniweka, maisha yangu hapa, nami . . . Na, jamani, mtu yeyote anajua ya kwamba jambo fulani lilinipata, nilikuwa gugu, Naye akanifanya ngano, si—sijui jinsi ilivyotokea." Nikasema, "Ingewezekanaje kamwe?"

199 Nami nikasema, "Nifanye nini, Bwana? Nina umri wa miaka hamsini, na—na mimi—mimi . . . Siku zangu zimehesabiwa, sina muda mrefu zaidi wa kukaa." Nikasema, "Nifanye nini nipate kukufanyia jambo fulani?"

Niliendelea kusikia Sauti ikisema, "Kaza mwendo."

200 Sasa, kumbukeni marafiki, hii *hapa* Biblia yangu, ikiwa mimi ni mlokole, sijui, jamani, kama ndivyo nilivyo, si—sijui lolote kulihusu, ni—ninaamini moyo wangu uko pamoja na Mungu, nami ninaamini amethibitisha hilo mbele zenu. Huenda nimekosea katika mambo fulani, lakini kama ndivyo ilivyo, ni—ni kukosea bila kujua. Mnaona?

201 Halafu basi, tulipokuwa . . . Ni—nilikuwa nikiwazia jambo hilo, nami nikaendelea kusikia Kitu fulani kikisema, "Kaza mwendo."

Nikasema, "Ni nani huyo?" Nikasema, "Lazima awe ni mke wangu." Nikasema, "Ulisema nini, Mpenzi?" Kamwe hakusogea.

Nikamtikisa, nikasema, "Meda?"

Akasema, "Huh?" Alikuwa amelala usingizi mzito.

Nami nikasema, "Vema, haikuwa ni yeye."

Nikasikiliza tena, ikasema, "Endelea kukaza mwendo."

202 Sasa, najua maono, hili lingeweza kuwa ni ono, kama lilikuwa, kamwe sikuwa na moja kama hilo. Nami nikasema, "Labda ni mimi ninayesema jambo hilo."

203 Kwa sababu wakati mmoja, nilikuwa nimelemewa na kuhuzunika sana nikienda mkutanoni, ndipo nikapiga magoti sakafuni nikiomba niondolewe mzigo huo, ndipo nikasikia mtu fulani akisimama mlangoni akichacharisha tu kitu fulani, akizungumza katika Kijerumani, ama kitu kama hicho. Nikawaza, "Vema, sijui huyo ni nani?" Nikaenda upesi, wala nisingeweza kumwona mtu yeyote. Nikawaza, "Vema, iko wapi?" Ilikuwa ni mimi, nikinena mwenyewe. Mnaona? Nami nikatulia tu kabisa mpaka ikaisha.

204 Na hapo ndipo mwanamke yule, mwajua, nyote mnajua habari zake, nadhani nimewaambia, aliyeponywa, alikuwa amelala kando ya barabara, akitokwa na damu kiasi cha kufa. Ndipo nusu saa baadaye, alikuwa pale mzima kabisa na mwenye afya, Roho Mtakatifu akifanya maombezi.

205 Halafu basi, nami nikawazia labda huenda ikawa ni mimi nikisema, "Endelea kukaza mwendo," kwa hiyo nikaweka kidole changu juu ya kinywa changu, namna *hii*.

Nikamsikia akisema, "Endelea kukaza mwendo, kukaza mwendo."

Nikasema, "U nani Wewe unayesema nami? Ni nani aliye katika chumba hiki?"

206 Na hivyo ndivyo inavyokuja, kama tu maono hapa, ni halisi tu, ni Sauti tu, kama tu vile mnavyoisikia yangu, kasema, "Endelea kukaza mwendo."

Nami nikasema, "Endelea kukaza mwendo?"

Kasema, "Thawabu kubwa iko tu mbele."

Nami nikasema, "Unamaanisha ng'ambo ya pazia?"

Kasema, "Naam." Kasema, "Je, ungependa kupaona?"

Nikasema, "Ningetaka, ingenisaidia kama tu ningeweza kuona."

207 Ndipo jambo fulani likatukia, nikajisikia nikiuacha mwili huu. Sasa, sikuwahi kuwa na ono kama hilo. Mimi, nikiangalia nyuma, nikijiona nimelala pale, nikiegemea kichwa cha kitanda huku nimeinua mikono yangu *hivi*. Mnaona? Nami nikajiangalia, nikawazia, "Ninakufa!"

208 Ndipo nikaanza kuondoka, na muda si muda mwajua, ni— nikafika mahali padogo ambapo palikaa kitu kama *hicho*. Na

mara nilipofika pale, hawa hapa maelfu ya watu wanakuja, na kila mtu alionekana kijana.

209 Sasa, mimi niko katika umati uliochangamana, mimi ni ndugu yenu, nanyi angalieni, nasema hivi katika Jina la Bwana: Kila mmoja wenu atakutana nami pale kama mtakuwa sahihi. Lakini hawa wasichana wadogo wakinijia, wakinikumbatia, na kupaza sauti, "Ndugu yangu wa thamani!"

210 Sasa angalieni, nimeninii...nilipokuwa mwenye dhambi, kamwe sikuzurura-zurura, sikuwa mchafu kuzurura na wanawake. Nami sijali jinsi mtu anavyojaribu kuishi kitakatifu, na jinsi anavyoishi kitauwa, kama mwanamke akimkumbatia mwanamume, ni mhemuko wa kibinadamu. Sasa, afadhali wewe...Sijali, unaweza kujiita umetakaswa, nami ninaamini katika utakaso, pia, lakini wewe ungali ni mwanadamu, sawa kabisa, na kuna mhemuko. Sisemi ungefanya makosa, la hasha, nguvu za Mungu hukuzuia, nawe unaendelea. Lakini hata katika Mahali hapo, mhemuko huo wa kibinadamu haukuwepo.

211 Basi hawa hapa wanakuja wakitupa tu mikono yao huku, wakisema, "Ndugu yangu mpendwa!" Hao wanawake wote walikuwa na nywele ndefu, nguo nyeupe, miguu bila viatu, walikuwa vijana, yapata, wanaonekana kuwa na umri wa kama miaka kumi na minane, ishirini. Mimi...Wangenishika na kunikumbatia kwa mikono yao, waseme, "Loo, ndugu yetu wa thamani," na kunikumbatia tu namna hiyo, na kuondoka, na mtu mwingine.

212 Nilimwona mke wangu wa kwanza akija. Sasa, alikufa alipokuwa na umri wa kama miaka ishirini na miwili, hakuwa amebadilika. Akaja mbio, nikasema, "Hakika, ataniita mume."

213 Ndipo akapanda, akaanza kutabasamu, akanikumbatia, akasema, "Ndugu yangu mpendwa!" Ndipo akamkumbatia mwanamke fulani ambaye alikuwa ndiyo kwanza anikumbatie, msichana fulani.

214 Kisha hawa hapa wanaume wakaja, walionekana kana kwamba walikuwa...walikuwa na nywele za matimutimu begani mwao, nao walikuwa watu wenye sura nzuri sana niliowahi kuona, macho kama nyota, meno meupe kama lulu, walikuwa wakinikumbatia, wakisema, "Loo, ndugu yetu wa thamani!"

215 Ndipo mmoja wao akampazia sauti huyo mwingine, kasema, "Wazia, amewasili! Hatimaye amewasili!"

216 Ndipo nikawazia, "Je, nimekufa, na hii ni...nimekuja Utukufuni? Ndio huu?" Nami nikawaza, "Haiwezekani."

217 Ndipo nikaangalia, na ile Sauti iliyokuwa imenena nami huko chini chumbani mwangu, nikaisikia tena. Nikaangalia nyuma, nami nikajiona nimelala pale kitandani. Sikuwahi

kupatwa na jambo kama hilo. Limenifanyia jambo fulani, siwezi kuwa vile vile tena.

218 Kwa hiyo basi ni—nikaangalia, nami nikawazia, "Ni kitu gani hiki?" Nikawaza, "Vema, watu hao wote wanaonekana ni vijana." Nami nikaangalia chini, nami nilikuwa kijana, ni—nilikuwa nimegeuka kuwa kijana tena. Nikasema, "Vema, ajabu hii." Nami nikaangalia na . . .

219 Siwezi kulielezea, hakuna maneno ninayoweza kuwazia. Kama ningesema *timilifu*, ama—ama—ama *kuu kabisa*, ama—ama *kamilifu*, hilo lisingeigusa. Wao—wao . . . Hakukuwako na kesho, hakukuwako na jana. Wao—wao—wao walikuwa katika Umilele. Nao hawakuchoka, haikuwalazimu kula, hata hivyo walikuwa na hisi, ningeweza kuwagusa, wangeweza kuzungumza, walikuwa wakiniangalia, walikuwa na hisi.

Nami nikasema, "Si—sielewi hili."

Ndipo Sauti hiyo ikasema, "Huu ni upendo mkamilifu." Kasema, "Hivyo si ndivyo ulivyosema Roho Mtakatifu alikuwa?"

Nikasema, "Naam."

"Basi huu ni upendo mkamilifu."

220 Na yapata wakati huo, kundi kubwa la watu likaniinua, na kunipeleka mahali fulani, na kunipandisha juu kidogo, kama ki—kibanda, ama kitu fulani. Na hawa hapa walikuwa watu, ningeweza kuwaona kwa makumi ya maelfu wakija kutoka kila mahali, kila mmoja kijana, mrembo, wakikimbia, wakinikumbatia.

Nikasema, "Vema, sielewi jambo hili."

221 Na papo hapo, msichana mrembo, akaja mbio, naye akasema, "Loo, ndugu yangu mpendwa!" Akasema, "Tuna furaha sana kukuona. Karibu!" Kisha akaondoka.

222 Nami nikasema, "Bwana asifiwe, dada." Nikaangalia kote. Ndipo nikawaza, "Ni nini hii? Ni kitu gani kinachoendelea? Imekuwaje?"

223 Mara tu Sauti ikasema, "Katika Biblia ambapo ilisema ya kwamba Yakobo alikusanyika pamoja na watu wake, na huyo mwingine, hii inafanana na hiyo, ambapo utakusanyika pamoja na nanii wako . . . ambapo *utakusanyika* pamoja na watu wako."

Nikasema, "Hao wote wa Branham?" Nikasema kwamba, "Si—sikuamini kamwe kulikuwako na wengi hivyo."

224 Akasema, "Hao si wa Branham." Kasema, "Hao ni waongofu wako, hao ni waongofu wako." Kasema, "Mwanamke huyo anayekuvutia," kasema, "unajua alikuwa na umri gani ulipomwongoza kwa Kristo?"

Nikasema, "Sina fununu."

Kasema, "Zaidi ya miaka tisini." Kasema, "Unaona, yeye ni kijana milele."

225 Ndipo akaniangalia, akasema, "Ndugu Branham, Yesu atakuja siku moja, kisha tutarudi duniani." Kisha kasema, "Ndipo tutaupokea mwili wetu uliotukuzwa, kisha tutaishi pamoja, milele."

Nikasema, "Lakini mimi. . .Kwa—kwa—kwa nini mnaniweka hapa juu?"

Wakasema, "Ulikuwa kiongozi, ulituongoza."

Nikasema, "Loo, hebu nimwone Yesu kama nimepita, ninataka kumwona."

226 Sauti hiyo ikasema, "Huwezi kumwona sasa." Kasema, "Atakuja, lakini kwanza atakuja kwako," kisha kasema, "atakuhukumu kwa Injili uliyohubiri."

Nami nikasema, "Ati Injili ninayohubiri?"

"Naam."

Nami nikasema, "Je, itamlazimu Mtakatifu Paulo kusimama mbele ya waongofu wake?"

Kasema, "Hakika, atafanya hivyo, pia."

227 Nikasema, "Sikubadilisha hata Neno moja, nilidumu jinsi hasa Biblia ilivyolisema. Sijali yale mtu yeyote alisema, ama hakusema, nilidumu moja kwa moja Nalo namna hiyo, kwa hiyo kama kundi la Paulo limeokoka, langu limeokoka, pia."

228 Ndipo ilionekana kama sauti kuu ya maelfu na maelfu ilisema, "Tunajua hilo!"

229 Nikasema, "Mungu asifiwe, kamwe sikupata kuwa na furaha hivyo kwamba nilidumu mwaminifu kwa hilo Neno." Mnaona? "Sijawahi kuwa na furaha hivyo."

230 Na papo hapo tu, nikaangalia. . .Miaka mingi iliyopita, nilikuwa na maskini mbwa wa kuwinda, jina lake lilikuwa Fritz, naye alikuwa nusu Airedale na nusu Newfoundland, alikuwa mbwa mkubwa mno. Naye alikuwa akiambatana nami kila mahali nilipoenda kuwinda, na ndicho kitu kizuri sana nilichopata kuwa nacho, angelala pamoja nami, naye akanivalisha nguo za shule kutokana na kuwinda, kuwafuata oposamu mitini, na cheche, na chochote kile nilichonasa, na kwa hiyo, alinivalisha tu nguo za shule. Nami ningalimwacha mahali popote, angeweza kwenda nyumbani peke yake.

231 Basi siku moja, tulipohamia mjini, polisi mmoja alikuja na kutupa kitanzi cha mbwa uani na kumwua. Nilipokuja nyumbani na kumzika, nilikuwa tu na umri wa miaka kumi na sita, kumi na saba, nilipopigapiga sehemu ya mwisho ya mavumbi pale, nilisema, "Fritz, nita—nita—nitamwua mtu huyo kwa kufanya hivyo," nikaingia nyumbani na kuchukua bunduki yangu, nikaanza kushuka kwenda kwenye kituo cha polisi kumtafuta.

232 Basi nilipofika barabarani, maskini Ford ndogo ikatokea nyuma yangu, ilikuwa ni baba yangu, alinyakua bunduki hiyo kutoka mkononi mwangu, alikuwa ni mtu mdogo, akanipiga kofi kichwani, kasema, "Ingia kwenye gari hilo."

233 Ndipo nikarudi, nami nikasema, "Fritz," nikaenda kwenye kaburi lake, nikasema, "Fritz, hivi ndivyo nitakavyofanya, kama Baba hataniruhusu kufanya hivyo, siku moja nitamkuta mtaani akitembea, nami nitapoteza udhibiti wa gari langu, ninakuahidi nitajilipizia kisasi," (Mnaona?) "kwa kukuua." Nami nililimaanisha.

234 Ndipo yapata mwaka mmoja baadaye, nikaokoka. Ndipo nikamwongoza mtu huyu kwa Mungu, na kumzika baada ya yeye kuokoka, Bw. Short, yule polisi.

235 Maskini mbwa alikuwa ameondoka, sikuzote niliwazia baada ya kuokolewa, niliwazia, "Sijui nitakapofika Kule, kama nitamwona maskini Fritz." Halafu nilipokuwa nimeketi pale, niliangalia akija kuvuka kilima, naye huyu hapa maskini Fritz akinijia. Naye alikuwa tu akiuramba ulimi wake mwajua, na kuhema namna hiyo, akiniangalia. Nikaangalia na huyu hapa maskini Prince akija nyuma yake, farasi wangu, farasi wangu wa matandiko, naye akanikimbilia, akaniwekelea shingo yake.

Nami nikasema, "Ee Mungu, ni kitu gani hiki?"

236 Mara Sauti ikanena na kusema, "Wote uliopata kuwapenda, na wote waliopata kukupenda, Mungu amekupa, sote tuko hapa pamoja." Loo, jamani! Moyo wangu ukayeyuka tu ndani yangu. "Wote uliopata kuwapenda, na wote waliopata kukupenda, wamekusanyika hapa pamoja nawe kukutana na Mungu."

237 Nikasema, "Loo, Mungu asifiwe!" Na yapata wakati huo, nilijisikia nikisogea. Nikasema, "Si lazima nirudi, sivyo?" Nami nikaendelea . . . Na katika dakika moja tu, nilikuwa huko nyuma kitandani tena.

238 Rafiki, mauti hayambadilishi mwanadamu, hubadilisha tu makao yako. Nina mke, mke mzuri sana, aliyeketi pale pale, nina watoto watatu wadogo, wasichana wawili wadogo, mvulana mdogo, na Billy Paul, ninataka kuwaishia, bali kusudi langu la kwanza ni kumwishia Kristo, kwa huduma yangu.

239 La pili: Ningetaka kuishi muda mrefu vya kutosha hata ningeweza kumwona mtoto wangu Joseph aliyeketi pale akiwa mhudumu, achukue roho nitakayomwachia. Roho yangu na ije juu yake. Nilipomweka wakfu kwa Mungu, akisimama pale mikononi mwa mama yake, sijui, kulikuwa na watoto kumi ama kumi na watano, nilipomchukua, Roho alinishika, na kusema, "Joseph, mwanangu, wewe ni nabii." Mungu, jalia roho yangu ije katika sehemu maradufu juu ya mwanangu.

240 Nitakapofika mwisho wa safari, wala siwezi kuendelea mbele zaidi, ninataka kumwachia Joseph Biblia hii, na kusema,

"Mpenzi, hasha, usipatane juu ya Neno moja, dumu mwaminifu kwa Mungu, kama itagharimu kila kitu kilichopo, wewe dumu mwaminifu kwa Mungu." Nitakapoweza kuona, kufanya hivyo, na kumwona Joseph akichukua Biblia yangu na kwenda mimbarani kama mtumishi wa Mungu aliyetiwa mafuta, yote yakitendeka basi, yote ninayoweza kumfanyia Mungu, itakuwa ni siku ya furaha.

241 Ninapojua ya kwamba ganda hili la kale, lenye makunyanzi, lililochakaa linaweza kubadilishwa, kuvuja katika jengo hili la kale, uhai ukivuja kutoka kwake, kuna Nyumba bora zaidi ng'ambo ya mto, kule.

242 Sikilizeni, enyi marafiki, popote Hapo palipo, hakuna pumzi moja kati yetu na hapo usiku wa leo. Kwa moyo wangu wote, hii ndiyo mara ya kwanza nimewahi kusimulia haya nje ya kanisa langu mwenyewe, kwa moyo wangu wote, kwa neema ya Mungu, kwa yote niwezayo kufanya, ninamwahidi Mungu nitamvuta kila mtu ikiwa nitafaulu, na kumshurutisha, na kadhalika amjie Yesu Kristo. Kwa kuwa huo ulikuwa ni wakati wa jinsi gani wakati hao watu, hao wanawake na wanaume wenye macho maangavu wakisimama pale, huku wamenikumbatia, wakipaza sauti, "Ndugu yangu mpendwa," na kujua ya kwamba huduma yangu ilikuwa ndiyo chanzo cha wao kuwa kule! Mungu anisaidie milele kuwaleta watu kwa Kristo, ndilo ombi langu.

Na tuombe.

243 Baba wa Mbinguni, kwa kuwa sasa tuko kwenye kilele chenyewe cha mkutano huu, tuko hapa katika kongamano pamoja na ndugu zetu, pamoja na ndugu wa thamani, Bwana, wanaoamini Injili hii, wahubiri hawa wa Full Gospel waliosimama barabarani, wengi wao hapa, nilipokuwa mvulana mwenye dhambi, wakihubiri Neno lili hili, na ubatizo wa Roho. Mama wengi wakongwe, wenye nywele zenye mvi hapa wamevunja mahindi, na—na kujaribu kuwapikia watoto wake ugali, na kuwapimia chakula mezani kujaribu kuisukuma Injili, nao hawa hapa wameketi usiku wa leo, wazee na wenye mvi, wengi wao wamechoka, wameinama mabega. Nimewapa mikono hapa kwenye uwanja huu, nami ninajua wapo hapa.

244 Ee Mungu, jalia tu wajue kwamba pumzi moja tu baada ya huu kuondoka hapa, watarudi kuwa vijana wanaume na wanawake wapate kuishi milele katika Nchi ambamo hakutakuwa na mvi wala kunyanzi, ambapo hakutakuwa na ugonjwa wala huzuni. Loo, napatamani Mahali hapo patukufu, popote pale, Bwana, nilipokuwa usiku huo, ama, asubuhi hiyo!

245 Ninaomba Mungu, ya kwamba kila mtu hapa, anisikie, Ee Mungu, kama nimewahi kupata neema machoni Pako, jalia maombi yangu yajibiwe, jalia kila mtu aliye hapa kwenye maeneo haya, jalia nikutane nao, kila mmoja, kule katika Mahali hapo patukufu, popote palipokuwa, ama chochote kilichokuwa,

Bwana. Jalia nikutane nao Mahali hapo. Ninawapenda, nao wananipenda, na Wewe uliniambia, Bwana, "Wote uliopata kuwapenda, na wote waliokupenda wamekusanyika hapa wawe pamoja nawe."

246 Ee Mungu, jalia kwamba huo umati utaongezeka kwa mamilioni. Tujalie, Baba. Uturehemu. Nijalie kamwe, maishani mwangu mwote, Bwana, kamwe nisipatane kwa Neno moja la Biblia hii, maana ninajua, kwanza nitahukumiwa, na hatima yao ya Milele inategemea hilo. Nisaidie, Bwana, jalia niwe mwaminifu na mkweli, na—na kuwaambia watu ya kwamba hawana budi kujazwa na Roho Mtakatifu, tujalie, Bwana. Hawana budi kuzaliwa mara ya pili. Tujalie.

247 Tusaidie, utusamehe dhambi zetu. Mungu, usiku wa leo, kuna wanaume na wanawake hapa walioinua mikono yao, hawakuwa na Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana, kwamba huu utakuwa ndio usiku, huu utakuwa ndio wakati, ambapo kutakuwako na roho fulani itakayowashika, roho ya shauku kubwa na kiu. "Heri ninyi mkiwa na njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa."

248 Ulisema hivyo, Bwana, ululiahidi, ninakunukulia Neno Lako, Bwana, kama wana njaa na kiu, Wewe uliahidi ungewajaza, nami ninaamini kila Neno ulilosema ni kweli. Bwana, jalia wajazwe usiku wa leo. Tujalie, Bwana.

249 Kama mwenye dhambi fulani alikuwa hapa, na kwa namna fulani alidanganya kwenye dhamira yake mwenyewe muda mfupi uliopita, dhamira ya mwanamume ama mwanamke huyo, wanajua ya kwamba wao ni wenye dhambi, wala hawakuinua mikono yao, Mungu, waaibishe, waite kutoka nyuma ya kichaka, uwafunike na ngozi ya—ya Bwana Yesu, kifuniko Chake, Roho. Alikuwa amevikwa na—na kuingizwa ndani ya nyumba na Roho Mtakatifu. Jalia hilo lije juu yao usiku wa leo, Bwana, liwashawishi. Jalia watoke na kufanya kongamano pamoja Nawe, na wapatanishwe na Mungu kupitia Damu ya Yesu Kristo. Tujalie, Bwana, naomba, katika Jina la Yesu.

250 Na huku tumeinamisha vichwa vyetu: Je, kuna wenye dhambi, wenye dhambi wowote hapa, wangetaka kuja hapa kwa dakika moja tu? Labda hili huenda lisiwasaidie, bali nataka kuwa na hakika na jambo hili. Nimewaambia ukweli halisi, basi nisaidie, Mungu anajua hilo. Ninataka kuwa na hakika ya kwamba hakuna mwenye dhambi uwanjani. Hebu niseme hivi: ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI: "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuingia katika Ufalme."

251 Na kama uko hapa usiku wa leo, na ROHO WA MUNGU ASEMA HIVI aliye ndani yangu, ninasema kweli, sisemi uongo, kitu kile kile kinacholithibitisha ni kurudi kwa Roho huyo wa kinabii anayeyapambanua mawazo, anayekwambia kile umefanya, kile utakachofanya, kile kitakachokupata, kila shida,

kila wakati kikamilifu, mwaka baada ya mwaka. Hilo ndilo thibitisho kwamba nimewaambia kweli, ya kwamba hii . . .

252 Neno la Bwana lilimjia nani? Nabii. Alikuwa na Neno la Bwana. Usisikilize wazo fulani la jani la mtini, njoo uamini, njoo upokee. Naye Yesu Kristo, ambaye ni Hakimu wangu, anajua ya kwamba nimewaambia, ya kwamba nilienda Mahali fulani palipokuwa na utukufu, ambapo wazee wanakuwa vijana, ambapo wanaishi milele na kamwe hawafi, na wakiwa pamoja na ahadi ya kurudi duniani kupokea mwili uliotukuzwa. Mungu anajua hiyo ni kweli.

253 Ninakualika, rafiki yangu mwenye dhambi, tafadhali, hebu nikusihi, hebu nikushawishi, ikiwa kupiga magoti kwangu kutasaidia, kama ni kulia, ikiwa kushawishi kutasaidia, hebu nikushawishi: Msiende njia yoyote nyingine, bali njoni kwa Yesu sasa, wazee kwa vijana, na mpatanishwe na Mungu.

254 Ninasimama hapa kama mhudumu wa Injili, tayari kukushika mkono na kukuombea. Waweza kuja hapa sasa kwangu, na tuombe pamoja, rafiki mwenye dhambi? Hata uwe nani, kijana au mzee, ninangojea kukupokea. Je, utakuja sasa, wakati kukiwako na wakati wa neema, na wakati ambao Mungu anakuita?

255 Mungu awabariki, ninawaona wawili, mwanamume na mwanamke wakija mbele, wakishuka moja kwa moja. Ndugu Joseph, kama utasogea kwa muda kidogo tu hapo, na kumwacha ndugu aje apitie moja kwa moja hapa, na huyo dada.

256 Je, mwenye dhambi mwingine, naweza kukushawishi? Je, utakuja upatanishwe na Mungu? Huyu hapa mvulana mdogo na msichana mdogo wanakuja.

257 Ninasema kweli katika Kristo, sisemi uongo. Hakuna mtu anayeweza kuchukua Fundisho ninalohubiri na kulikanusha, hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo, sijawahi kuona mtu yeyote angeweza kufanya hivyo, ni kweli ya Injili. Upambanuzi wa Roho ni mkamilifu, hakuna mtu anayeweza kusema kamwe kwamba haujapata kuwa mkamilifu. Nami nitawaambia sasa, kuna Mahali pakamilifu, Mbingu kamilifu, Mungu mkamilifu, Mwokozi mkamilifu, Damu kamilifu, Upatanisho mkamilifu, kiumbe kikamilifu kwa ajili yenu.

258 Sasa, kama wewe ni mfuasi wa kanisa, na umefanya tu maungamo, yaondoe hayo majani ya mtini kutoka kwako usiku wa leo, kuja hapa mbele ya kusanyiko hili, simama hapa ili niweze kuomba pamoja nawe. Hivi utakuja? Angalia tu watu wakikusanyika hapa sasa.

259 Haya hapa aliyosema Yesu: "Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu." Wanakuja hapa kusimama karibu na . . . Huyu hapa mtu hata kwenye mikongojo akijaribu kupanda vipandio. Hilo linapaswa kuwaaibisha baadhi yenu mnaoweza kutembea,

mkaja bila magongo. Jalia ashuke bila magongo, ndilo ombi langu.

260 Njoni, baadhi yenu mnaweza kuja huku, njoni huku, njoni huku juu, na mje hapa. Hivi mtakuja? Ninakungojea. Mungu akubariki, ndugu yangu. Njoo moja kwa moja hapo. Je, wenye dhambi wengine wangesimama tu na kuja? Hebu niwashawishi, katika Jina la Kristo.

261 Hawa hapa mume na mke wazee wanakuja wameshikana mikono. Jinsi hilo lilivyo tamu kujua, hata katika umri huu, wanakuja sasa wapate kupatanishwa na Mungu. Sikilizeni, niangalieni, kama hawa mume na mke hapa wanaokuja kwa uaminifu mkubwa, nasema hivi katika Jina la Bwana Yesu: Kama wanakuja kwa uaminifu mkuu, nitakutana nao katika Nchi nyingine watakapokuwa mume na mke vijana tena na kuwapa mkono.

262 Loo, ukipita juu yake, ni rahisi sana. Mungu hakulifanya gumu, ati kanuni nyingi sana zinazokubidi kujifunza. Mnajua kile tunachojaribu kufanya?

263 Mtu fulani anasema, "Nifanye nini nipate kuokolewa?"

264 Unasema, "Huna budi kuacha kuvuta sigara, huna budi kuacha kunywa pombe." Tunawaambia kile wanachopaswa kuacha kufanya.

265 Paulo alimwambia kile alichopaswa kufanya, "Mwamini Bwana Yesu Kristo." Hivyo tu. Si kile unachopaswa *kuacha* kufanya, kile unachopaswa *kufanya* upate kuokolewa. Amini kwanza, mambo haya mengine yanajishughulikia yenyewe, wewe amini kwanza.

266 Utakuja, ewe mwenye dhambi? Nitangojea tu kwa muda kidogo zaidi, maana kabla sijainuka kutoka kwenye kile kitanda, nilimtikisa mke wangu, ameketi papo hapo sasa, alikuwa angali amelala, nami nikamtikisa, nikasema, "Mpenzi?"

Akasema, "Nini?"

Nikasema, "Jambo fulani limetukia." Nami nikamwambia.

267 Nikatoka kitandani. Kuna picha ya Yesu juu tu ya kitanda changu, upande *huu* kuna mikono inayoomba niliyochongewa huko Ujerumani, ukumbusho, upande mwingine ni kibanda kidogo nilichokuwa nikiishi, msanii fulani wa Kijerumani alikichora kwenye turubai, moja kwa moja upande huu mwingine ni ile picha ya Malaika wa Bwana amesimama juu ya . . . mna picha Yake, wengi wenu. Nikaangalia juu, nikasema, "Mbele za Mungu, mbele za Kristo, mbele ya Jeshi la Mbinguni, ninakuahidi, Mungu, kuwashawishi, na kuwasihi, na—na hata kuwashurutisha watu waje. Kwa kuwa hata ikinibidi kuwafanya wanikasirikie kidogo sasa . . . "

268 Jinsi yule mwanamke mwenye umri wa miaka tisini, katika urembo wa msichana aliyesimama pale, akiniangalia, kasema, “Loo, ndugu yangu wa thamani!”

269 Ndipo Yule aliyekuwa akizungumza nami akasema, “Sababu ya yeye kusema hivyo, alikuwa amepita umri wa miaka tisini ulipomwongoza kwa Yesu, sasa hawezi kamwe kuzeeka, wala kufa, tena.” Si ajabu alikuwa na shukrani.

270 Hivi hutakuja? Kuna mwingine? Kuna mwingine mmoja tu angesimama? Ninajisikia tu kusukumwa kwa namna fulani, kwamba si—si—sifanyi vizuri niwezavyo. Njoo, hebu nikushawishi, hebu nikuombe uje. Kuna mwingine? Kuna mwingine? Mtu fulani angesimama tu, na kusema, “Naam, ndugu mhubiri, ninataka kuja sasa. Ninaamini kila neno ulilosema ni kweli, ninakuja kupatanishwa na Mungu.”

271 Ninyi nyote, marafiki zangu wa thamani, kuanzia mvulana huyu mdogo kote kote kufikia mtu huyu wa makamu, ninawaahidi kwa uaminifu, nimewaambia kweli. Mungu na anipige kama sijawaambia kweli. Mnaona? Hiyo ni kweli. Nimekuwa mwaminifu kwenu. Nitakutana nanyi tena, kama kweli ninyi ni waaminifu, nitakutana nanyi tena katika Nchi ambamo nyote mtakuwa vijana, ambapo mauti yametoweka. Ninanena katika Jina la Bwana Yesu, sisemi uongo. Hiyo ni kweli.

272 Sasa, ulikuja, Kitu fulani kilikuvuta, Kitu fulani kilisema, “Njoo.” Natumaini Mungu atakufanya mhubiri, mwanangu, ninatumaini, ambaye ataichukua Injili, baada ya labda kuja kwenye kaburi la Ndugu Branham siku moja, na kusema, “Naam, alizungumza nami usiku mmoja huko Chautauqua, huko Ohio.” Na awajalie, enyi wavulana wadogo, wasichana wadogo.

273 Ni wangapi hapa ambao hawajampokea Roho Mtakatifu? Je, ungetaka kuja na kusimama papa hapa tunapoomba? Njoo tu kwa ajili ya maombi.

274 Kumbukeni, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuingia katika Ufalme. Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu. . . ”

275 Sidhani tuna nafasi kwa ajili yao hapa, Ndugu Sullivan, ninawataka tu wajaze marefu ya kanisa hapo. Hebu kidogo, ninataka kuomba. Na—na—na—nataka hili lifanywe vizuri, nataka lifanywe ipasavyo. Umesema kweli, najua, Ndugu Sullivan, usingemruhusu mtu yeyote ndani mle isipokuwa yule angekuwa mwalimu halisi katika chumba hiki, hilo ni zuri. Haya yote yameshughulikiwa na watu watauwa.

276 Sasa, hatuwahukumu, hatuihukumu dini yenu, kusema Presbiteri, au Methodisti, au Baptisti, hilo ni sawa, Mungu awabariki Presbiteri, Methodisti, na Baptisti. Lakini unataka kuwa Mpresbiteri, Mmethodisti, na Mbatisti na uwe na Roho Mtakatifu, hivyo ndivyo unavyotaka, unaona. Chochote ulicho,

unataka kuwa Kristo. Wewe kaa na kanisa lako, hilo ni sawa, utakuwa nuru katika kanisa hilo kuwaongoza wengine.

277 Hebu niwaambie, marafiki, hamjui furaha ni nini, kumbukeni, mpaka mtakapokuwa mmevuka ile Nchi huko ng'ambo, na muone kweli ni kitu gani. Angalieni, ningefanya hivi kama mtumishi wa Kristo? Ninaweka Biblia hii juu ya moyo wangu, na kusema, nina . . . Haingeweza kuingia . . . Kama hiyo ilikuwa ni moja, Mbingu ya kwanza niliyojaliwa kuiona, naye Paulo alinyakuliwa hata Mbingu ya tatu, aliona nini?

278 Si ajabu yeye alisema, "Jicho halijaona, sikio halijasikia, wala hayajaingia katika moyo wa mwanadamu, yale Mungu aliyowawekea, akiba, wampendao."

279 Unasema basi, "Ndugu Branham, Paulo alisema hatuna budi kumwamini Bwana Yesu Kristo."

280 Hiyo ni kweli, lakini Paulo *pia* alisema, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini? Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

281 Hilo ndilo swali linalofuata. Sasa, unataka kumpokea Roho Mtakatifu, sivyo? Watu hawa wanataka kuokolewa, mnataka kumpokea Roho Mtakatifu.

282 Sasa, hao tu ndio wanaokuja? Hao ndio wote humu jengoni, ama kwenye jengo ambao hawana Roho Mtakatifu? Vema.

283 Sasa, kama Mungu hutimiza ahadi Yake, ninaweza kuthibitisha jambo hili dakika hii, Roho Mtakatifu anaweza kusimama hapa na kuita kundi la watu katika kusanyiko hili na kuzungumza nao. Ni karama tu. Inakubidi tu, jikabidhi tu kwa Mungu na umngojee, nayo itaanza kunena. Ninyi nyote . . . Wangapi wameona hilo likifanywa? Bila shaka mmeona, usiku baada ya usiku. Ninasema kweli.

284 Sasa, kama wewe ni mwaminifu, nawe unaamini hili kwa moyo wako wote, utampokea Roho Mtakatifu, utampokea. Sasa, usijali kama mtu fulani yuko karibu nawe, labda anafanya jambo *moja*, mtu mwingine . . . Usiwaangalie, wewe iangalie Dhabihu. Mnaenda kufanya kongamano, mtalizungumzia na Mungu sasa hivi, mfanye kongamano, "Bwana, Kitu fulani kiliniambia ninahitaji Roho Mtakatifu. Mimi hapa nipate kumpokea. Fungua madirisha, Bwana, niko tayari kwa ajili Yake."

285 Na kwako wewe hapa, "Bwana, ninataka ku—ninataka kuwa mtoto Wako, sasa ninampokea Yesu kama Mwokozi wangu binafsi." Mtafanya hivyo, kila mmoja wenu? Je, kila mmoja . . . ? Utampokea, mwanangu, kama Mwokozi wako? Ninyi karibu hapo? Mtampokea kama Mwokozi wenu, nyote mlio hapa? Vema.

286 Je, unataka kumpokea Roho Mtakatifu? Unaenda kufanya kongamano sasa, kumpokea Roho Mtakatifu? Hiyo ni kweli,

mwinulie Mungu mkono wako. “Ninaingia kumpokea Roho Mtakatifu.”

287 Wote wanaotaka kumpenda Yesu, inua mkono wako, “Ninataka kumtumikia, nitampokea sasa hivi. Hakuna kitu ninachoweza kufanya, ninamkubali kama Mwokozi wangu, Mtu aliyekufa kwa ajili yangu.”

288 Sasa, ningethubutu kukuacha utoke hapa, bila mimi kuwa na hakika, hakika ya kibinadamu kadiri nilivyoweza, kwamba Mungu. . .? Ninataka kukutana nanyi huko ng’ambo. Ninataka kukutana nanyi watoto, nataka kukutana nanyi watu, nataka kukutana nanyi.

289 Sasa, kwa moyo wangu wote, nitaomba. Nami ninataka kila mmoja katika jengo hili mwinamishe vichwa vyenu, ninawatakeni msijaribu kuondoka sasa. Tutawaombea wagonjwa katika dakika chache. Nami ninawatakeni mwinamishe vichwa vyenu, nami nawatakeni mwombe pamoja nami ya kwamba Mungu atawaokoa watu hawa hapa. Ninaamini moyo wangu, kwa yote yaliyo ndani yangu, tayari wameokoka, nitamtolea tu Mungu shukrani. Tayari wamemkubali Yesu, wameinua mikono yao kwamba walitaka. . . walimkubali kama Mwokozi.

290 “Na yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, hataingia Hukumuni kamwe, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Hiyo ni Biblia.

291 Lakini ninawatakeni mwombe, ninawatakeni mumshukuru Mungu. Ndipo sote tutaenda hapa katika chumba hiki kingine hapa, na kukaa humo mpaka jambo fulani litukie. Na tuinamishe vichwa vyetu kila mahali, ombeni pamoja nami, ninyi watu wote watakatifu, kwa njia yako mwenyewe chini ya moyo wako, waombee watu hawa.

292 Mpendwa Yesu, ninajuaje, huenda haya yakawa ndiyo mahubiri ya mwisho nitakayowahi kutoa, hii huenda ikawa ndiyo nafasi yangu ya mwisho kumwita mwenye dhambi atubu. Sijui, Bwana, ninatumaini ya kwamba nitaweza kwa miaka mingi kulifanya, hata utakapokuja, kama hilo linawezekana na linaruhusiwa Kwako. Lakini hawa hapa vijana, wenye umri wa makamu, na wazee, wamesimama jukwaani, kwa unyenyekevu, kwa utamu, hata kwa watoto hawa wadogo wenye macho yaliyofifishwa kwa machozi, wakija kukupokea Wewe kama Mwokozi wao. Ulisema hivi katika Neno Lako Mwenyewe: “Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe.”

293 Basi wao ni Wako, Bwana, wao ndio kumbukumbu za ujumbe usiku wa leo; wao ni Wako, kwa sababu Yesu alikufa. Wewe ulisema, “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu,

hakuna mmoja wao atakayepotea. Nitampa Uzima wa Milele, nitamfufua katika siku ya mwisho." Hilo ni Neno Lako, Bwana.

294 Ulisema ya kwamba "Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, hataingia kamwe hukumuni, ama kuhukumiwa, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

295 Bwana, nimewaita, Roho Mtakatifu alisema nao, waliitikia na wakaja, sasa wao ni Wako, Bwana, ninawakabidhi Kwako wakati—wakati Mungu akiwakabidhi kwa Yesu kama karama za upendo wa neema Yake. Wabariki, Bwana. Jalia niweze katika Nchi ile, ambako Wewe ulinipeleka hivi majuzi, kuwaona watu hawa tena, kuwapa mikono. Jinsi watakavyoikumbatia shingo yangu, nami nitakumbatia zao, nikiita, "ndugu na dada!" Jinsi maisha ya kale, ya kimwili, ya dhambi yatakavyotoweka, wala asili yote ya kale ya dhambi haitakuwako tena, nasi kweli tutakuwa ndugu na dada wasioghoshiwa! Huo utakuwa ni wakati wa jinsi gani, Mungu! Jalia uje upesi, Bwana Yesu, uje upesi.

296 Wageuze watu hawa usiku wa leo, Baba, tunaomba. Wote uliowaita Wewe ulisema umewahesabia haki, na wote uliowahesabia haki, uliwatukuza. Ninaomba ya kwamba watakuwa Wako tangu sasa, ninawakabidhi mikononi Mwako, katika Jina la Yesu, Mwanao.

297 Hapa wamesimama wengi kuizunguka madhabahu hii, chini ya reli hii, wanaume na wanawake, wavulana kwa wasichana, ambao wame—wamekukubali Wewe kama Mwokozi binafsi. Wanataka kujazwa na Roho Mtakatifu; Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste ahadi ilikuwa kwa ajili yao. Nasi tunaona ni kweli katika kila wakati na kote tangu wakati huo, kwamba mtu yeyote atakayekuja akiwa na kiu na njaa, kamwe humkatai, daima Wewe humjaza, unalitimiza Neno Lako. Ninaomba, Mungu, usiku wa leo, kwa moyo wangu wote, kwa yote yaliyo ndani yangu, usiache hata mmoja wa hawa...ninawadai kila mmoja kwa ajili Yako.

298 Shetani, ewe roho mwenye mashaka, ewe ibilisi usiyeamini, ninakuapisha katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu mwenye haki, uwaondokee!

299 Jalia Roho Mtakatifu wa Mungu awashukie usiku huu, na jalia wajazwe na Roho Mtakatifu wa Mungu. Kila mmoja wao aje kwenye uwanja huu kesho, akihubiri Injili, akishuhudia, akienda kila mahali, kueneza habari kila mahali ya kwamba Roho Mtakatifu angali ni halisi. Tujalie, Bwana.

300 Ninawakabidhi Kwako kwa maombi yangu maaminifu, Nalo lilisema, "Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii," wakati mamia ya wanaume wenye haki hapa ndani, na wanawake, wanapoomba, Mungu, wapokee. Tunawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

301 Vema, kiongozi, papa hapa kuna mtu hapa wa kuwaongoza, geukeni moja kwa moja upande huu sasa kwenye chumba cha maombi. Wewe shuka moja kwa moja upande huu sasa, ndugu, dada. Huyo ndugu aliye na kidonda cha mguu hapo, wewe njoo huku, nafikiri ndiyo njia ya kushuka chini. Hivi huwezi kutengeneza pazia hilo papo hapo, ili waweze kuingia humo? Vema, Ndugu Sullivan atalishughulikia hilo.

302 Nendeni moja kwa moja upande huu sasa, kwa ajili ya—kwa ajili ya—kwa ajili ya ibada ya kutafuta, ibada ya kungojea. Usitoke humo. Wewe ingia humo ukiyakinia . . .

Useme, "Nimechoka."

Huyo ni ibilisi.

Unasema, "Ninaingia, natumaini nitampata usiku wa leo."

Huyo bado ni ibilisi.

303 "Ninaingia ili kumpata, kwa sababu Mungu alinipa, Yeye aliniahidi, nami ninamfuatilia. Nitafanya kongamano, nami nitakaa katika kongamano hili mpaka Mungu atakapokuja na kunijibu." Hiyo ndiyo njia. "Mungu, usiponipa Roho Mtakatifu, utanikuta nimelala hapa nimekufa." Hiyo ni . . . Kuwa mwaminifu, Mungu atakuwa mwaminifu kwako.

Nampenda, nampenda
Kwani . . .

( . . . ? . . . papo hapo. Rudi moja kwa moja ukampokee. Yuko pale pale akikungojea ambapo wewe . . . )

304 Nilipata tu kitu kitamu. Maskini huyu kipenzi mrembo, mwenye nywele za shaba, karibu kama mtoto wangu Sarah aliyeketi pale, alisema, "Ndugu Branham, nilitaka tu kukwambia jambo fulani. Ulipokuwa hapa . . ." Ilikuwa ni mwaka jana, kipenzi? Nilipokuwa hapa wakati ule mwingine? Alikuwa na uvimbe mwilini mwake mwote, kasema nilimwombea, ndipo uvimbe wote ukatoka, basi usiku wa leo alijisikia anapaswa kuja kuyatoa maisha yake kwa Yesu. Nautakia heri maskini moyo wake. Mungu akubariki, kipenzi. Rudini moja kwa moja nyuma . . . Baadhi yenu . . . ? . . . mwonyesheni njia pale pale. Nautakia heri maskini moyo wake.

Nampenda, (Loo, jamani!)
. . . Yeye . . .

Hebu tuinue mikono yetu.

. . . alinipenda
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

305 Hebu tuuvumishe. Loo, Jina Lake lisifiwe. Jinsi hilo linavyoufurahisha moyo wangu!

. . . wokovu wangu
Mtini Kalvari.

306 Hivi hamna furaha mlifanya kongamano pamoja Naye si muda mrefu uliopita? Hivi huna furaha kwamba Yeye alikuwa pale kukujibu, kukutia muhuri hata Siku ya Ukombozi wako kwa muhuri wa neema Yake na Roho Wake?

307 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, rafiki wa thamani sana, rafiki mzee mhubiri, huko nyuma nilipokuwa katika kanisa la Kibaptisti, akasema, "Ndugu Branham, Ibrahimu alimwamini Mungu, ndipo akahesabiwa kwamba ana haki."

Nikasema, "Hiyo ni kweli, Daktari."

Akasema, "Ibrahimu angeweza kufanya nini zaidi ila kuamini?"

308 Nikasema, "Hakuna, bali Mungu alimpa muhuri wa tohara kama thibitisho la kupatanishwa kwa imani yake."

309 Nikasema, "Hivi Yeye amewahi kukutia muhuri, Daktari, kwa Roho Mtakatifu?" Unaona? "Kama ukisema una imani wala Yeye kamwe hajakupa Roho Mtakatifu bado, Yeye kamwe hajaitambua imani yako. Unaona? Baada ya Ibrahimu kumwamini Mungu, Mungu alimpa muhuri wa tohara kama ishara ya kwamba alikuwa amempatanisha, ama, kuitambua imani yake."

310 Kama ukisema, "Ninamwamini Mungu," Yeye kamwe hajakupa Roho Mtakatifu, Yeye kamwe hajakutambua bado, kungali kuna kitu kinachoning'inia. Lakini anapokupa Roho Mtakatifu, amekutia muhuri hata Siku ya Ukombozi wako. Loo, jamani, hakuna cha kuhofia, tembea tu na kupaza sauti, "Nampenda."

311 Loo jamani, mara moja tu zaidi, hilo linasikika zuri sana. Sikilizeni, hilo si linasikika zuri? Kufa!

312 Unasema, "Ati linasikika zuri kwa watu kufa?"

313 Naam, napenda kuwasikia wakifa namna hiyo. Amina. Bwana alisema, "Ina thamani machoni Pake mauti ya watakatifu Wake." Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli. Ninapenda kuwasikia wakifa namna hiyo, wanajifia wenyewe. Naam, bwana.

314 Unasema, "Wanajitahidi sana."

315 Vema, wanakufa kwa shida, hivyo tu. Lakini wao—wao kweli watakufa, kisha watazaliwa mara ya pili, upya. Amina.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

316 Nilikuwa nikiangalia chini kuona, nilikuwa nimewacheleweshsha, nikawaza, "Nitaomba msamaha." Nikawaza, "La. Paulo alihubiri Injili ii hii usiku kucha usiku mmoja, mvulana mmoja akaanguka kutoka darini, akafa.

Paulo akaenda akaulaza mwili wake juu yake, maana alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu, akalaza mwili wake juu yake, kasema, 'Uhai wake unamrudia, kila kitu ni sawa.'"

317 Ni wangapi hapa walio na Roho Mtakatifu? Vema, wangapi ni wagonjwa? Inueni mikono yenu. Vema, ninyi mlio na Roho Mtakatifu, wekeaneni mikono; Roho Mtakatifu yule yule aliyekuwa ndani ya Paulo yuko ndani yenu, Injili ile ile inahubiriwa kwa nguvu zile zile, hakusema, "Ishara hii itafuatana na wahubiri." Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na *hao* waaminio, kila mmoja wao."

318 Wekeaneni mikono, na kuombeana sasa, angalieni kinachotukia. Dada, ndugu, kwenye viti hivyo vya magurudumu, na kadhalika, vipi kuhusu hilo? Hebu hii iwe ndiyo saa. Ndugu Boze, wawekee mikono hao watu hapo. Baadhi yenu wengine, ombeaneni, ndivyo hivyo. Ninyi nyote ni wahubiri, maombi, mmejazwa na Roho Mtakatifu.

319 Mungu, katika Jina la Yesu, mimina Roho Wako juu ya watu hawa, mtume Roho Mtakatifu katika nguvu kuu, uwape upako. Waponye watu hawa ambao leso hizi na kadhalika zinawakilisha. Tujalie, Bwana. Jalia Roho Wako na nguvu Zako ziingie ndani ya watu hawa, jalia waombeane maombi ya imani. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

320 Hili ni kongamano, jalia Roho Mtakatifu aje na kulitikisa hili jengo ambamo tumekusanyika pamoja, na magonjwa yote na kadhalika yaondoke na kuwatoka watu hawa. Ninamhukumu ibilisi na kazi zake zote, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

60-0608 Kufanya Makongamano
Miami Valley Chautauqua Campgrounds
Chautauqua, Ohio Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org